# DHANA YA ULINGANIFU KATIKA TAFSIRI YA FASIHI; TATHMINI YA USALITI MJINI

NA

**MWANIKI, P. NYAGA**

**C50/70532/2007**

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI, KITIVO CHA SANAA; IDARA YA ISIMU NA LUGHA

KATIKA

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2009

University of NAIROBI Library
0479623 1

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa na mtu mwingine kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A. katika Chuo Kingine chochote.

Mwaniki Peter Nyaga

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kwa mtihani chini ya usimamizi wetu, sisi tulioteuliwa kuisimamia.

Dkt. Mwenda Mbatiah

(Msimamizi)

Dkt. Zaja Omboga

(Msimamizi)

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa Zakaria Mwaniki aliyenitunza vyema na marehemu mama yangu Nerea Wambeti ambaye mawaidha yake ya kiusomi ningali nayakumbuka.

Natabaruku pia kwa mpenzi wangu Rachael; watoto wangu Ben na Brian. Nashukuru sana kwa kuvumilia hali ya ukiwa nilipokuwa mbali nanyi.

# SHUKRANI

Natoa shukrani nyingi na za dhati kwa mwenyezi mungu kwa kunipa uwezo na akili ya kuyamudu masomo yangu katika upeo kama huu. Shukrani nyingi za dhati ziwafikie wote walionisaidia kwa namna tofauti katika mchakato wote wa masomo yangu. Kwanza kabisa shukrani nyingi ziwaendee wasimamizi wangu, Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Zaja Omboga ambao waliniongoza vyema kwa kujitolea kwa hali na mali hadi nilipojua nilichohitajika kufanya.

Nawapa shukrani pia wahadhiri katika idara ya Isimu na lugha za Kiafrika wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao ni Prof. Kithaka wa mberia, Prof. Mohammed H. Abdulaziz, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. John Habwe, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Tom Olali na Bw. Mungania. Ubingwa wenu katika lugha na fasihi uliniwezesha kupiga hatua nyingi za kiusomi.

Kwa wakufunzi wenzangu Josphat Gitonga, Lina Akaka, Geofrey Mukabane, Mary Ndungu, Margaret Mwachanya na Josphine Murila. Nashukuru sana kwa muda wote tuliokuwa pamoja na kunifaidi kwa mambo mengi. Nawatakieni kila la heri maishani. Wenzangu waliokuwa nyuma au mbele yangu nawapa pongezi. Hawa ni kama vile Eunice, Caroline na Emily.

Marafiki na jamaa zangu walionitakia heri na fanaka nawashukuru kwa moyo wangu wote. Mugendi Muta, pokea shukrani za kipekee kwa kuwa ndugu na rafiki aliyenifaa sana kuishi Nairobi pamoja na ukarimu wa bibi yako mama Ngatha. Nawashukuru dada na ndugu zangu Rwamba, Wanjuki, Mukami, Lucy, Njeru Muturi, Njoki na Wangai, Shukrani za dhati ziwaendee wajomba na binamu zangu kama vile Muta, Riunga, Muchangi, Njeru, Kariuki. Natoa shukrani pia kwa mashemeji zangu kama vile Kiarago, Elija, Muriithi na Selina. Hali kadhalika nawashukuru marafiki Wily, Ken, Njoka Tim, Waweru, Baba na mama Wanja, Kirimi, Kamuti, Jim, kariuki Mutua, Muthuri, Kariuki, Njiru, Kago, Kopro Ireri, Mwaniki, Herman, Bw. Na Bi. Ireli Mutongoria, Walter, Susy na Kariuki Grace.

Shukrani ziwafikie wote ambao sikuwataja hapa lakini siwezi kumsahau aliyenipigia chapa tasnifu hii. Mueni kwa Ustadi na Uvumilivu Mwingi. Ahsanteni nyote. Heri na fanaka ziwashukie.

# YALIYOMO

Mada ..... i

Ikirari ..... ii

Tabaruku ..... iii

Shukrani ..... iv

Yaliyomo ..... vi

Vifupisho ..... viii

Muhtasari ..... ix

SURA YA KWANZA ..... 1

1.0 Utangulizi ..... 1

1.1 Tatizo linalotafitiwa ..... 2

1.2 Madhumuni ya Utafiti ..... 3

1.3 Nadharia Tete ..... 6

1.4 Sababu za Kuchagua mada hii ..... 6

1.5 Upeo na Mipaka ..... 8

1.6 Msingi wa nadharia ya Utafiti ..... 9

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ..... 13

1.8 Njia za Utafiti ..... 21

SURA YA PILI: FAFANUZI ZA ULINGANIFU ..... 22

2.0 Utangulizi ..... 22

2.1 Dhana ya Ulinganifu ..... 22

2.2 Aina za Ulinganifu ..... 29

2.2.1 Ulinganifu wa Kiumbo ..... 29

2.2.2 Ulinganifu wa Uamili ..... 32

2.2.3 Ulinganifu wa Kimuktadha ..... 35

2.2.4 Ulinganifu wa Kitamathali ..... 37

2.2.5 Ulinganifu wa Lugha kisarufi na Kisintaksia ..... 39

2.2.6 Ulinganifu wa Kiisimu ..... 41

2.2.7 Ulinganifu wa Kimaudhui ..... 47

2.2.8 Hitimisho ..... 50

SURA YA TATU: TATHMINI YA AINA ZA ULINGANIFU ..... 51

3.1 Utangulizi ..... 51

3.2 Ulinganifu wa Kiumbo ..... 51

3.3 Ulinganifu wa Uamili ..... 55

3.4 Ulinganifu wa Kimuktadha ..... 57

3.5 Ulinganifu wa Kitamathali ..... 60

3.6 Ulinganifu wa Lugha, Kisarufi na Kisintaksia ..... 62

3.7 Ulinganifu wa Kiisimu ..... 66

3.8 Ulinganifu wa Kimaudhui ..... 69

SURA YA NNE: ..... 73

4.0 Hitimisho ..... 73

MAREJELEO ..... 77

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| MC | - | Matini Chanzi |
| ML | - | Matini Lengwa |
| LC | - | Lugha Chanzi |
| LL | - | Lugha Lengwa |
| HC | - | Hadhira Chanzi |
| HL | - | Hadhira Lengwa |

# MUHTASARI

Tasnifu hii inashughulikia tafsiri ya kazi ya kifasihi iliyotafsiriwa kutoka kiingereza hadi kiswahili. Tumetumia matini za *Betrayal in the City* (1976) na *Usaliti Mjini* (1994).

Utafiti wetu umechunguza jinsi dhana ya aina za ulinganifu inaweza kuwepo au kutokuwepo katika kazi zilizotafsiriwa.

Tasnifu hii imejengeka katika sura nne. Sura ya kwanza tumetoa somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, misingi ya kinadharia, nadharia tete na vilevile tumerejelea yaliyoandikwa kuhusu somo letu la utafiti.

Katika sura ya Pili tumezingatia fafanuzi za dhana ya ulinganifu pamoja na kujadili aina mbalimbali za ulinganifu.

Sura ya tatu ndicho kiini cha utafiti huu ambapo tumechunguza aina za ulinganifu katika kazi ya kifasihi ya *Usaliti Mjini*. Tumejadili ulinganifu wa kimaumbo, kiuamili, kisarufi, kitamathali, kiisimu, kimuktadha na kimaudhui.

Sura ya nne ni hitimisho. Tumeeleza matokeo ya utafiti wetu na athari zake na kisha tukatoa mapendekezo yetu.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Suala la ulinganifu wa maana katika taaluma ya tafsiri ni suala ambalo limekuwepo kwa muda mrefu. Dhana nzima ya ulinganifu imekuwa ikiongoza na kushawishi sio tu na utekelezi wa tafsiri bali pia usomaji na utafiti wake. Katika tafiti nyingi zilizokwishafanywa katika fasihi ya Kiswahili na kwingineko, suala hili la ulinganifu limekuwa likisisitizwa na kupewa kipaumbele hata kama uelewa wake umekuwa jambo la mjadala. Tafiti nyingi zimekuwa zikikazania kuwepo kwa ulinganifu kati ya kazi chanzi na kazi lengwa katika hali ambapo uhalisi wa kutafsiri hauonekani kuunga mkono au hata kuwezesha kuwepo kwa ulinganifu, hususan katika tafsiri za kifasihi.

Hata kama tafiti nyingi zimekuwa zikisisitiza haja ya kuwepo kwa ulinganifu kati ya kazi chanzi na kazi lengwa, kujenga ulinganifu katika miktadha lengwa ni kazi ngumu, tata na telezi. Isitoshe, tafiti na mielekeo ya kiusomi inayosisitiza kuwepo kwa ulinganifu katika tafsiri, ama inapuuza uhalisi wa kutafsiri fasihi au haijaonyesha ni kwa nini kuna lazima hiyo au kuonyesha ulinganifu huo ni kwa manufaa ya nani. Tafiti za kipembuzi za miaka ya hivi karibuni zimebaini kwamba ulinganifu ni dhana fumbati-dhana iliyofumbata na kusomba mambo mengi

yakiwemo ulinganifu wa maana ya kimsamiati, ulinganifu wa miktadha, ulinganifu wa matarajio, ulinganifu wa hadhira, ulinganifu wa kiuamili na mengineyo. Kuwepo kwa mambo haya na mengine mengi ni ithibati kwamba ulinganifu ni dhana changamano inayohitaji kuangaliwa upya hasa kwa jinsi inavyopasa kutumika katika tafsiri kwa sababu, dosari za mchakato mzima wa kutafsiri zaweza kuzalisha tafsiri iliyo na lugha isiyo na mantiki, mnato wala ufasaha. Haya yangeepukwa kama dhana ya ulinganifu ingeeleweka vizuri ili kutathimini mchango wake katika kazi zilizotafsiriwa.

Katika utafitu wetu, tutajadili ulinganifu wa kimaumbo, kileksia, kisarufi, kisemantiki na vipengele fulani vya utamaduni katika ***Usaliti Mjini.*** Tutatumia tafsiri ya *Usaliti Mjini* ili kuonyesha vile ilivyo vigumu kuwa na ulinganifu wa kijumla katika kazi za fasihi ya Kiswahili zilozotafsiriwa.

## 1.1 TATIZO LINALOTAFITIWA

Tatizo linaloshughulikiwa katika utafiti huu ni kujadili dhana ya ulinganifu katika tafsiri kwa kujikita katika misingi dhahiri. Hata kama kunaonekana kuwepo na uhalali wa kusisitiza kuwepo kwa ulinganifu wa kimaana kati ya kazi chanzi na kazi lengwa, mara nyingi uhalisi wa michakato na miktadha ya kutafsiri unakwenda kinyume na misisitizo hii. Kwa hivyo utafiti huu utajikita katika kujadili aina mbalimbali za ulinganifu. Kwa mfano, kuzungumza juu ya ulinganifu

wa maumbo ya lugha na ulinganifu wa miktadha ya upokezi, badala ya kuzungumza kijumla juu ya ulinganifu wa maana.

Tafiti nyingi za fasihi tafsiri zilizofanywa katika fasihi ya Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni kama vile Ali (1981), Shitemi (1990), Mutie (1997), Onguko (1999), na Mulila (2005) zimezungumzia kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya kazi chanzi na kazi lengwa. Kazi hizi zinapoangaliwa kwa pamoja, inadhihirika kwamba ulinganifu unaozungumziwa ni jambo la kijumla na wala sio dhana iliyoelezwa kwa kina ili kuangaza jambo au suala dhahiri. Katika hali kama hizi, dhana ya ulinganifu inapowekwa katika mizani, haijulikani ni ulinganifu wa maana gani unaofaa kupewa kipaumbele-ulinganifu wa maana ya maneno, ulinganifu wa maana ya utamaduni, maana ya uamili, na kadhalika. Kwa maoni ya Zaja (2006: 72) suala la ulinganifu ni suala ambalo linahitaji kuondelewa katika misingi ya kiumbo na kiisimu na badala yake kuangaliwa katika mkabala wa uamili.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Nia hasa ya utafiti huu ni kuonyesha jinsi ambavyo dhana hii ya ulinganifu ilivyo tata, isiyokuwa na uelewa wa aina moja au hata ufafanuzi halisi, jinsi ilivyowahi kushawishi usomi na utafiti mbalimbali, na kwa kufanya hivyo ikaishia kujenga uelewa potovu wa malengo ya tafsiri. Kutafuta kujenga ulinganifu katika kila kazi ya fasihi tafsiri kumekuwa na athari ya kufilisha na kusukuma pembeni

mambo kadha wa kadha ya kimsingi yanayohitaji pia kushughulikiwa katika usomi na tafiti za fasihi tafsiri kwa jumla. Uelewa wa aina hii katika mikabala ya nadharia za sasa katika tafsiri unaweza kutiliwa shaka, ya kwanza ikiwa ni kung'ang'ania kujenga ulinganifu katika kila tafsiri ya fasihi ni kizuizi katika kufikia ufanisi, ubunifu au uelewa mpya na upeo wa juu wa masuala ya fasihi tafsiri.

Katika kiwango kingine, tafiti zote zinazong'ang'ania kuwepo kwa ulinganifu kati ya kazi chanzi na kazi lengwa, hasa pale ambapo ulinganifu unaozungumziwa haujafafanuliwa na kudhihirisha maana dhahiri, tafiti hizi zinapuuza uhalisi mwingi wa kutafsiri fasihi. Kwa mfano, tafiti hizi hazionyeshi ni kwa jinsi gani ulinganifu unawezekana kati ya lugha mbili tofauti-lugha zilizo na mifumo tofauti ya kiisimu tamaduni tofauti, mitazamo tofauti ya kilimwengu, historia na utamaduni tofauti wa kiusomi, hadhira tofauti na matarajio tofauti ya hadhira. Kwa kupuuza mambo kama haya na mengine kama haya, haiwezi kujulikana ulinganifu ni nini. Ili kudhihirisha ukweli wa madai haya, utafiti huu unalenga kuonyesha fafanuzi anuwai za ulinganifu- kuanzia ulinganifu wa kiisimu, ulinganifu wa kiumbo, ulinganifu wa miundo, mitindo ya matumizi ya lugha, ulinganifu wa kiuamili, ulinganifu wa miktadha (kiwakati na kijiografia) ulinganifu wa kitamaduni, ulinganifu wa maudhui na ulinganifu wa hadhira.

Kwa kujikita katika uhalisi huu, utafiti huu unalenga kuonyesha kwamba kuna sababu za aina mbalimbali zinazoweza kutumiwa kueleza kuwepo au kutokuwepo kwa ulinganifu katika tafsiri za fasihi. Baadhi ya sababu za kimsingi zinazochangia kutokuwepo kwa ulinganifu ni pamoja na kutambua kwamba tafsiri zinachochewa na sababu nyingi na zinatekelezwa kutimiza malengo mengi. Kwa hivyo, zinatekelezwa kwa kutumia mikabala mingi tofauti. Kwa mfano, kuna mikabala ya tafsiri za moja kwa moja, tafsiri zenye vyanzo vingi lakini ambazo hujenga matini moja katika miktadha lengwa, tafsiri teuzi ambazo huteua baadhi ya sehemu za kazi chanzi na kuacha sehemu nyingine, kuna tafsiri za urekebishaji au usahihishaji zinazofanywa ili kusahihisha misimamo au uelewa fulani, tafsiri afiki zinazofanywa kupanua upokezi, tafsiri changanuzi na kadhalika. Mbali na aina hizi za tafsiri, kuna pia uhalisi wa kumkutadhisha, yaani kuiwajibikia miktadha lengwa kwa kila namna.

Ithibati za kuhimili mijadala hii zitatolewa katika tamthilia ya *Usaliti Mjini* tafsiri ya Adaka Kisia na Josephat Wasyatsa (1994). Baadhi ya mambo muhimu yatakayodhihirishwa katika uchanganuzi wa kazi hii ni kuonyesha jinsi ambavyo kujenga ulinganifu kunavyoweza kugeuka kuwa kizuizi cha kufanikisha mawasiliano ya wazi katika tafsiri badala ya kuangaliwa kama ufanisi. Utafiti huu utaongozwa malengo yafutayo:

1. Kuchunguza ufanisi wa kutafsiri kama jambo linalotegemea uelewa wa kina wa dhana ya ulinganifu.

2. Kubainisha matatizo na kasoro za tafsiri zinazojitokeza katika tafsiri ya *Usaliti Mjini* ambazo zinahusishwa na uelewa potovu wa dhana ya ulinganifu.
3. Kuchunguza kama nadharia ya mwitiko wa msomaji inaweza kutumika katika kujadili dhana ya ulinganifu kwa kujikita katika kazi ya kifasihi ya *Usaliti Mjini.*

## 1.3 NADHARIA TETE

1. Ufanisi wa kutafsiri na uwezo wa kutambua makosa yanayoweza kuzuia ufanisi huo ni mambo yanayotegemea uelewa wa kina wa dhana ya ulinganifu.
2. Matatizo na kasoro za tafsiri zinazojitokeza katika tafsiri ya *Usaliti Mjini* zinaweza kuhusishwa na uelewa potovu wa dhana ya ulinganifu.
3. Nadharia ya kifasihi ya mwitiko wa msomaji inaweza kutumika katika kujadili dhana ya ulinganifu kwa kujikita katika kazi ya kifasihi ya *Usaliti Mjini.*

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Kuna sababu nyingi zizazochochea uteuzi wa mada hii. Sababu moja ya kimsingi ni kutaka kuonyesha jinsi kung'ang'ania kujenga ulinganifu katika tafsiri kunaweza kuwa kizuizi na kikwazo kikubwa badala ya kuwa lengo la manufaa katika mchakato mzima wa kutafsiri. Ulinganifu ambao umezungumziwa katika

tafiti zilizofanywa katika fasihi ya Kiswahili umekuwa ukionyesha yaliyowezekana katika kazi chanzi bila ya kuona uwezekano au mawezekano yaliyoko katika kazi lengwa na katika lugha lengwa ambayo yanaweza kuwa chanzo cha mafunzo na maarifa mengi kwa ujumla.

Sababu nyingine inayotoa motisha kutafiti mada hii inahusiana na ukweli kwamba dhana ya ulinganifu katika tafiti za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili imekuwa ikishughulikiwa katika misingi ya maana za kijumla bila kubainisha ni ulinganifu gani unaokusudiwa kwamba watafiti wengi wamekuwa wakisema hakuna ulinganifu bila kubainisha ni ulinganifu gani unaozungumziwa. Maana za kijumla zimekuwa zikibana maana kwamba dhana ya ulinganifu inaweza kuangaliwa katika viwango mbalimbali jambo linalofungamana na ukweli kwamba katika miongo ya hivi karibuni kumeibuka nadharia na mitazamo ya kihakiki inayotambua kwamba licha ya maana hizo za kijumla za ulinganifu kuna uwezekano wa kuzungumzia aina maalum au dhahiri za ulinganifu.

Kwa upande mwingine, tafiti nyingi zimekuwa zikiegemea kutafuta udhaifu unaojitokeza katika kazi lengwa jambo ambalo halisaidii kazi hizo lengwa kupata nafasi maalum katika tafsiri (Shitemi 1990). Kutokana na sababu hizi ni dhahiri kwamba ulinganifu ni dhana inayostahili kutafitiwa lakini kwa kutumia mitazamo na mielekeo mipya inayotambua kwamba ulinganifu ni kitu kipana ambacho hakiwezi kushungulikiwa katika ujumla wake. Badala yake ulinganifu unastahili

kuangaliwa katika misingi ya maswala dhahiri ili kuyadhihirisha maswala haya dhahiri, tutatumia kazi ya *Usaliti Mjini* kama kitovu chetu cha data ya msingi

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu unanuia kutafiti dhana ya ulinganifu kama inavyojitokeza katika tafsiri za fasihi ya Kiswahili hususan tamthilia ya *Usaliti Mjini* hasa kama ilivyotafsiriwa na Adaka Kisia na Josephat Wasyatsa (1994). Utafiti huu utajishughulisha na aina saba za ulinganifu ambazo ni ulinganifu wa kiisimu, ulinganifu wa kiumbo, ulinganifu wa lugha kisarufi na kisintaksia, ulinganifu wa kitamathali, ulinganifu wa uamili, ulinganifu wa kimaudhui na ulinganifu wa kimuktadha.

Tutaonyesha sababu zinazochangia kuwepo au kutowepo kwa ulinganifu kama vile aina ya tafsiri na matarajio ya hadhira inayohusika, na kisha kutathmini mafanikio ya *Usaliti Mjini* katika misingi hiyo ya ulinganifu. Utafiti huu pia utajikita katika kueleza ulinganifu sio kwa nia ya kulaumu na kuhukumu kazi moja kwa moja kuwa mbaya na nyingine kuwa nzuri, lakini kwa nia ya kueleza ni kwa nini kazi za kifasihi katika miktadha ya tafsiri haziwezi kulingana. Hali kadhalika kutakuwa na umuhimu kuonyesha kwamba kutokuwepo kwa ulinganifu hakuwezi kuinyima kazi lengwa usomekaji na uibukaji wa ufasiri badalia.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA YA UTAFITI

Mijadala na mahitimisho yatakayotolewa katika utafiti huu kwa kiasi kikubwa yataongozwa na kuegemezwa katika nadharia ya mwitiko wa msomaji. Nadharia ya mwitiko wa msomaji ni nadharia iliyoanza kupata umaarufu na kushamiri mnamo miaka ya 1970, lakini mianzo ya kuchipuka kwake inarudi nyuma hadi miaka ya 1920 hadi 1930. Hata hivyo, suala la jinsi wasomaji wanavyoingiliana na kwa hivyo wanavyoathiriwa na kushawishiwa na kazi za kifasihi na kisanaa kwa jumla ni jambo linalokwenda nyuma hadi siku za Plato na Aristotle.

Nadharia ya mwitiko wa msomaji ni nadharia inayohusika na utathmini wa nafasi ya msomaji katika kuikamilisha kazi ya kifasihi. Katika nadharia ya mwitiko wa msomaji, inaaminika kwamba uhusika wa msomaji ni muhimu kama ulivyo uhusika wa mwandishi au uhusika wa taratibu za kiuandishi, lakini zaidi ya hayo, kuibuka kwa maana ya kazi ya kifasihi kunahusishwa zaidi na msomaji. Hali hizi zote zinaonyesha ni kwa nini hapawezi kuwepo na ulinganifu wa maana. Kwa hivyo, hakuna matini inayoweza kuchochea maana moja, vile vile hakuna ufasiri mmoja unaoweza kuchukuliwa kuwa sahihi zaidi kuliko miitiko mingine.

Waasisi wa nadharia ya mwitiko wa msomaji wanashikilia kwamba maana ya kazi ya kifasihi haiwezi kuwa ya aina moja tu kila wakati na katika kila muktadha. Hii ni kwa sababu wasomaji ni watu walio na tajriba anuwai na kila

wanaposoma tajriba zao zinashawishi maana inayojitokeza. Katika misingi hiyo hiyo, nadharia hii inasisitiza kwamba kubainika kwa maana ya kazi ya kifasihi kunategemea mwingiliano ulioko kati ya mwandishi, taratibu za kiuandishi, taratibu za kimatini na uwezo na tajriba za msomaji.

Mbali na nadharia ya mwitiko wa msomaji kumpa kipaumbele msomaji, nadharia hii pia inajali jukumu la mwandishi katika ujenzi wa maana na ushawishi wa ufasiri wa maana hiyo. Pamoja na kumwangaza msomaji, nadharia hii pia inamulika mchakato wote wa kusoma hasa kwa nia ya kutaka kuielewa tajriba nzima inayoletwa na msomaji katika usomaji wake kama vile-sababu au lengo la usomaji wake, maarifa aliyonayo juu ya mada inayozungumziwa, umilisi alionao wa elementi za kiisimu za lugha husika, nadharia kadha wa kadha zinazomwongoza, haya yote ni mambo yanayoshawishi ufasiri wa kazi inayosomwa na yanatofautiana kutoka kwa msomaji mmoja hadi mwingine.

Nadharia ya mwitiko wa msomaji ina mikabala kadha wa kadha ya uchanganuzi. Hii ni pamoja na mkabala wa kumulika wasomaji kwa sababu nadharia hii inaamini kwamba kusoma ni maingiliano kati ya matini na msomaji na kwamba uibukaji wa maana unatokana na kitendo hiki cha kusoma. (msomaji + matini = maana). Hata hivyo, usomaji na uibukaji wa maana kutoka matini yoyote ile ni mambo yanayochangiwa na mambo mengi kama vile uzoevu wa msomaji,

misimamo ya kijinsia, uana, asili, umri, tabaka, chukulizi zake juu ya mambo ya maisha, hisia na taathira za kiasasi.

Kuna mkabala wa kuangaza miitiko ya wasomaji kwamba mwitiko wowote wa msomaji mbali na kushawishiwa na tajriba za msomaji, unategemea pia uwezo wa msomaji. Miitiko ni jambo linalohusishwa na nadharia za kifasihi za Kimarekani za uhakiki mpya za miaka ya 1930-1950. Moja ya mambo yanayoangazwa katika uhakiki mpya ni umuhimu wa maneno katika uandishi wowote. Mkabala huu unatambua kwamba maneno hayo yanawavuta wasomaji kwa njia zinazotofautiana. Kwa kufanya hivyo, msomaji huwa si mpokezi tuli wa maarifa lakini huwa mhusika mtendaji katika uundaji wa maana ya matini husika.

Kuna pia mkabala wa umuundo unaojishughulisha na jinsi miundo ya kimatini inavyowezesha kubainika kwa maana. Mifumo au vichocheo ndani ya matini ni sehemu ya mfumo mkubwa unaoruhusu maana kutokea katika nguzo zote za jamii fasihi ikiwemo. Kwa mfano, tunaposikia king'ora cha gari ya wazima moto lazima tuipishe njia kuonyesha vile jamii hutoa njia za kufasili na kuleta utengamano duniani. Kwa mujibu wa wanamuundo, msomaji huwa ameamua kabla ya kusoma matini mfumo atakaotumia kuyakinisha maana kama vile mbinu ya kuchanganua hadithi kwa kutumia elementi zote zinazohusika kuisimulia hususan msimulizi, sauti, mtindo, kikundi kitenzi na hadhira.

Katika nadharia ya mwitiko wa msomaji kuna pia mkabala wa fenomenolojia wanaoamini matini na msomaji huchukua nafasi sawa katika mchakato wa kufasiri. Kutokana na haya matini huwa na uwezekano wa kuwa na ufasiri tofauti kila wakati msomaji anapoingiliana na matini huku akijiwekea matarajio yake kuhusu kitakachotendeka au kinyume cha haya. Matarajio haya hubadilikabadilika kwa kuwa hadithi yoyote hutuelekeza kwenye mgogoro au mvutano wa kidrama unaoleta upotezaji, huzuni, furaha, hofu na wakati mwingine kutimizwa kwa mahitaji ya msomaji. Wahakiki wanaotumia mwelekeo huu wanaamini kuwa maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Kutokana na haya msomaji anachukuliwa kama anayetoa mchango mkubwa katika uundaji wa maana. Utafiti huu utaongozwa na mkabala huu wa fenomenolojia.

Mkabala mwingine ni uhakiki wa kibinafsi. Kulingana na mkabala huu, nafasi ya wahakiki, mawazo, imani na tajiriba yao huchukua nafasi kubwa kuliko matini yenyewe katika utambuzi wa maana. Msomaji hubadilisha matini katika ulimwengu wa kibinafsi ambapo anachunguza (kupitia nafsi yake) uwezo wa kubuni unaopatanishwa na matini ili kukubalika katika jamii na kwa hivyo kuna fasiri kadha wa kadha kulingana na wasomaji tofauti. Mikabala hii mitatu Mathalan Umuundo, fenomenolojia na uhakiki wa kibinafsi ya mwitiko wa msomaji zote zinatambua umuhimu wa msomaji wa kazi yoyote ile ya kifasihi katika uundaji wa maana.

Uelewa wa madai haya ya nadharia ya mwitiko wa msomaji ni kigezo cha kimsingi katika kueleza dhana ya ulinganifu katika tafsiri za kifasihi. Kwanza, kitendo chochote cha kutafsiri kinaanza na usomaji wa matini chanzi. Mtafsiri, licha ya kuwa msomaji ni mtu binafsi aliye na tajriba anuwai anazozileta katika usomaji wake na kwa katika matini lengwa aliyotafsiri. Ni muhimu kuelewa suala zima la mtafsiri kama msomaji, kuelewa jinsi maana inavyombainikia na jinsi anavyoiwasilisha katika matini lengwa. Kuna haja pia kuelewa sababu zinazochochea tafsiri, mielekeo inayoongoza jinsi kazi fulani inavyotafsiriwa.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Nida (1964). Mwana anthropolojia na mtaalam wa isimu katika tafsiri za kibibilia alisisitiza kwamba kuna lazima ya kuwa na ulinganifu wa kitamaduni katika tafsiri ili kuhifadhi usahihi na uasilia wa neno takatifu. Nida alisisitiza kwamba njia moja ya kufanya hivi ni kufanya uchanganuzi wa kitamaduni wa maneno hayo. Hii kwa maoni ya Nida ndio njia moja ya hakika inayowezesha ujenzi wa ulinganifu wa maana za kitamaduni katika tafsiri. Mawazo haya ya Nida yalikuwa na ushawishi mkubwa katika tafiti nyingi za tafsiri katika miaka ya 1960 na hata baadaye na yalipata kuungwa mkono na wataalam kama vile Catford (1965). Umuhimu wa maandishi ya Nida katika utafiti huu ni kwamba mawazo yake ni miongoni mwa chanzo cha uelewa changamano wa dhana ya ulinganifu kama ilivyoeleweka wakati huo na baadaye.

Suala hili la ulinganifu limezungumziwa na Nida na Charles (1969) katika kitabu chao *The Theory and Practice of Translation* ambapo wanasisitiza umuhimu wa kuhifadhi Ulinganifu kuliko kuhifadhi ujumbe ulio katika matini chanzi. Ulinganifu wanaozungumzia ni ulinganifu wa kitamaduni katika tafsiri za kibibilia. Ulinganifu wa aina hii haukushughulikiwa katika ulinganifu wa kijumla, ni ulinganifu dhahiri kwamba viwango vya maana, vivuli vya maana na mitazamo ya maana wanayojishughulisha nayo ni mitazamo inayoelekeana na uhifadhi wa maana za kitamaduni. Katika hali kama hizi kuna udhahiri unaohusishwa na ulinganifu, tofauti na ambavyo imekuwa ikitokea katika tafsiri za fasihi ya Kiswahili. Mitazamo hii ya Nida na Charles japo haisemi waziwazi inatutahadharisha kuepuka kuishghulikia dhana ya ulinganifu katika misingi ya kijumla. Huu ndio uelewa tunaokusudia kuufikisha katika utafiti huu.

Ulinganifu mwingine ambao umepata kushughulikiwa kuhusiana na tafsiri ni ulinganifu wa kimuktadha. Ulinganifu wa kimuktadha unatambua kwamba maana ya neno na lugha kwa jumla inaweza kushawashiwa pakubwa na muktadha. Sambamba na utambuzi huo ni utambuzi mwingine kwamba mkutadha ni jambo linalofungamana na uhalisi wa matukio, uhalisi wa lugha husika, pamoja na uhalisi wa kitamaduni katika lugha hiyo. Haya ndiyo mambo yanayoshughulikiwa na Beekman na Callow (1974) katika kitabu chao *Transalating the word of God* Sababu ya kushughulikia kazi ya Beekman na Callow ni kwamba inaakisi malengo yetu ya kutambua kwamba ulinganifu wa kimaana hauwezi

kuzungumziwa nje ya mipaka ya ulinganifu wa kimuktadha. Mbali na kuakisi malengo yetu kazi hii inatoa ushahidi tunaoweza kuutumia kuonyesha kwamba haiwezekani kuzungumza juu ya ulinganifu bila kukita maana hiyo katika miktadha dhahiri.

Ulinganifu dhahiri umeweza kujadiliwa katika tafsiri kwa kushughulikia ulinganifu wa kisarufi, ulinganifu wa msamiati na ulinganifu wa kisemantiki. Guenthener F. na Guenthner. M. (1978) katika kitabu chao *Meaning and Translation* wameyajadili madai ya nadharia zinazohusu maana na tafsiri kwa kujikita katika maswala dhahiri hivyo tunapata ithibati ya kutosha kutokana na mchango wao kuwa dhana ya ulinganifu inaweza kushughulikiwa kwa kuingalia katika udhahiri wake mahususi badala ya kung'ang'ania kuitathimini kwa misingi ya kijumla.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Vingenevyo madai kama haya ya Guenthener na Guenthner. (1978) yamewahi kuchunguzwa kwa kuegemea ulinganifu wa msamiati kwa undani. Akijadili kuhusu utekelezi wa ulinganifu wa msamiati, Kelly (1979) katika kitabu chake *The true Interpreter* anasema kuna njia tatu za kutafuta ulinganifu ambazo ni kuwa na udhabiti wa ulinganifu, ulinganifu wa elimumwendo ama kujumulisha aina hizi mbili za ulinganifu katika shughuli nzima ya kutafsiri. Maoni yake yanatupatia motisha wa kutosha wa kujadili dhana ya ulinganifu katika utafiti wetu tukiegemea ulinganifu dhahiri.

Suala hili la ulinganifu limejadiliwa pia na Larson, (1984) katika kitabu chake *Meaning Based Translation: A guide to Cross-Language Equivalance* ambapo ameieleza dhana ya tafsiri na semantiki kwa kina na kujadili hatua mbalimbali za kutafsiri huku akibainisha vipengele vya isimu kama vile msamiati na muundo wa lugha. Larson anasema mtafsiri huwa kila wakati akitafuta ulinganifu wa msamiati kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa ingawa huwa mchakato tata.

Ulinganifu wa kiutamaduni kuhusiana na tafsiri umepata kushughulikiwa pia na Newmark, P (1988) katika kitabu chake *A Text book of Translation.* Anabainisha ulinganifu wa aina hii kama hali ambapo neno la kitamaduni katika lugha chanzi linatafsiriwa kwa neno la kitamaduni katika lugha lengwa. Kwa maoni ya Newmark, kuna uwezekano wa kuwa na ulinganifu dhahiri katika tafsiri hivyo tukaonelea tuchukue mwelekeo kama huu wa kubainisha ulinganifu mahususi badala ya kujikita katika swala nzima la ulinganifu wa kijumla.

Mwelekeo wa Neurbert, A. na Shreve M.S. (1992) katika kitabu chao *Translation as Text* unasisitiza juhudi za kuleta ulinganifu wa kimawasiliano kutoka matini chanzi hadi matini lengwa kwa kuangalia michakato inayotekelezwa na binadamu. Neurbert na Shreve wanabainisha kwamba maneno ya lugha moja ni tofaouti na maneno ya lugha ya pili na kwa hivyo maneno hayawezi kulingana kimaana isipokuwa maneno yanayolenga taaluma za kiufundi na kisayansi. Ulinganifu kama huu unaweza tu kutokea katika kiwango cha kimatini lakini sio kiisimu.

Mwandishi mwingine aliyegusia swala la ulinganifu ni Mwansoko (1996) katika kitabu chake *Kitangulizi cha Tafsiri.* Mawazo yake ni kwamba, ujumbe au mawazo katika lugha chanzi na lugha lengwa sharti 'yalingane' kwa sababu usawa wa matini chanzi na matini lengwa hauwezekani kwa sababu za kiisimu, kiutamaduni, kihistoria na kimazingira zinazofanya iwe vigumu kufasiri mawazo ya lugha moja katika lugha nyingine bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana. Mwansoko amejadili kuhusu ulinganifu wa kiutamaduni kwa kuainisha vipengele mbalimbali vya kiutamaduni kama vile ekolojia, siasa, dini mila na desturi. Uelewa tunaodhamiria kuufikisha katika utafiti huu ni kuchukua mwelekeo wa kuishghulikia dhana ya ulinganifu katika misingi dhahiri.

Ulinganifu mwingine, uliowahi kurejelewa katika misingi mahususi ni ulinganifu wa muktadha na ulinganifu wa utamuduni ulioshughulikiwa na Cook, G. (2003) katika kitabu chake *Applied Linguistics.* Kwa maoni yake, wanaotumia lugha fulani hufanya hivyo katika hali mahususi kutegemea mambo kadhaa kama vile uhusiano wa wahusika, umri wao, jinsia, tabaka lao wakati na mahali kutokana na masiala haya, ni dhahiri kwamba Cook alijikita katika ulinganifu wa muktadha na utamaduni hivyo utafiti huu utakwepa ulinganifu wa kijumla na kushughulikia ulinganifu dhahiri.

Dhana ya ulinganifu imeweza kushughulikiwa na watafiti mbalimbali pia. Baadhi yao ni Ali (1981) katika tasnifu yake ya uzamili T*he Problem of Translating from*

*English to swahili as Exemplified by V.O.K. News Items* alikojikita katika matatizo yatokanayo na tafsiri katika taarifa za habari za idhaa ya Sauti ya Kenya huku akizama katika ulinganishi wa kiisimu na kuitalii lugha katika ngazi zake mbali mbali. Kwa maoni ya Ali, tafsiri mbaya zinaweza kukosa maana na mawasiliano yakakosa kuwepo katika kazi lengwa ikilinganishwa na kazi chanzi. Ali amejadili kwa kina makosa yanayojitokeza katika tafsiri mbaya kama vile kupotoshwa kwa mawasiliano na kwa njia hii ameegemea sana kuchukua mwelekeo wa ulinganifu wa kimawasiliano. Kwa upande wetu, ulinganifu ulio dhahiri kama huu uliojadiliwa na Ali utatekelezwa katika utafiti huu.

Suala la ulinganifu limejadiliwa pia na Zaja (1986) katika tasnifu yake ya Uzamili *Fasihi Tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili (matatizo na athari zake*) ambapo ametalii matatizo ya tafsiri na kuonyesha athari zake katika ukuzaji wa fasihi hasa ile ya Kiswahili. Kwa maoni yake, tafsiri mawasiliano huwa rahisi kueleweka, laini, nyepesi na huweka ujumbe wazi kwa kufungamana na mahitaji ya muktadha wa lugha inayohusika. Vinginevyo, tafsiri hujaribu kuepuka matatizo ya namna mbalimbali yanayoweza kukwamiza mawasiliano. Matatizo haya huwa ya aina mbili yale ya kimaana na yale ya kimaumbo hivyo ni muhimu kwa utafiti huu kujikita katika ulinganifu dhahiri na kuubana ulinganifu wa kijumla.

Ulinganifu mwingine ambao umepata kushughulikiwa kuhusiana na tafsiri katika kiwango cha uhakiki ni ulinganifu wa kimuktadha. Muktadha ni hali yoyote

inayozua haja ya matumizi ya lugha. Huu ndio ulinganifu ulioshughulikiwa na Shitemi (1990) katika tasnifu yake ya uzamili *Mawasiliano katika Tafsiri, uteuzi wa mtafsiri* alikojadili miktadha ya aina mbali mbali kama vile miktadha ya kisemantiki, kisarufi, kileksia na kadhalika umuhimu wa kazi ya Shitemi kwa utafiti huu ni kuwa kuna uwezekano wa kuijadili dhana ya ulinganifu katika vipengele dhahiri.

Maoni kama haya ya Shitemi yalijadiliwa na Mutie (1997) katika Tasnifu yake ya uzamii *Sanaa katika Tafsiri: matatizo na Athari zake* alipochunguza matatizo ya kuhamisha sanaa katika kazi zilizotafsiriwa kwa kurejelea tamthilia ya *Mizigo*. Mutie alilinganisha sanaa katika kazi mbili husika na kudhihirisha vile fani hudhoofika katika kazi lengwa tofauti na kazi chanzi. Kwa maoni yake, maudhui ya tafsiri hayaendelezwi vyema au ujumbe unaowasilishwa mara nyingi unapotea na kuleta ukosefu wa uthabiti katika uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa. Mtafiti huyu alijadili dhana ya ulinganifu katika viwango vya kiisimu, kimawasiliano, kimaana, kitamaduni na kimazingira hivyo utafiti wake ni ithibati yetu ya kutosha kuwa ulinganifu wa kijumla unaweza ukaepukwa na kujikita katika ulinganifu dhahiri.

Mawazo kama ya Zaja (1986) yalijadiliwa na Omondi (1999) akijikita katika dhana na matatizo ya tafsiri huku akitathimini kazi ya kifasihi ya *Risasi Zianzapo Kuchanua*. Omondi alizama katika dhana ya tafsiri kama vile tafsiri za moja kwa

moja, tafsiri maana, tafsiri mawasiliano na kadhalika. Vinginevyo, Omondi alijadili ulinganifu wa kiisimu, kimazingira, kiutamaduni na kimuktadha hivyo mwelekeo wake unafaa utafiti huu unaojikita hususan na ulinganifu dhahiri.

Mhakiki mwingine aliyegusia swala la ulinganifu katika tafsiri ni Mulila (2005) katika Tasnifu yake ya uzamili *Muala na mshikamano katika kiswahili umuhimu wake katika uchanganuzi wa riwaya ya vipuli vya figo.* Akichunguza vipengele vya mtindo, dhamira na matini, Mulila anasema kazi yoyote inayohusu kipengele cha kimtindo haina budi kuonyesha mchango wake katika kufanikisha dhamira na maudhui. Kwa maoni ya Mulila, matini isiyo na mpangilio wa kisarufi ufaao hukosa kuwasiliana na uteuzi wa msamiati huweza kuonyesha athari za kitabaka, kitamaduni na hata kijinsia, kwa kujikita katika mawazo haya, ni dhahiri kuwa ulinganifu wa kijumla hauna bundi kuepukwa.

Swala la ulinganifu katika lugha ya Kiswahili limekuwa likishughulikiwa na wasomi wa kifasihi kwa chukulizi mbili kwa maoni ya Zaja (2006) katika tasnifu yake ya uzamifu *Siting Text, Culture, context and Pedagogy in Literary Translation: A Theorization in Cultural Transfer with example from selected texts in Kiswahili.* Moja kati ya hizi chukulizi ni kuwa kuwepo kwa matini takatifu katika lugha fulani ambayo inatafsiriwa kunaifanya itafsiriwe kwa uaminifu mkubwa. Matokeo ya mchakato kama huu huenda yakatupatia tafsiri ambayo imelinganisha neno moja na lingine kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Kwa

hivyo, itakuwa ni sawa na kuchukua mwelekeo wa ulinganifu wa kijumla bila kujikita katika ulinganifu dhahiri kama vile ulinganifu wa kitamaduni na wa kiisimu sawa na kusudio la utafiti huu.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Katika utafiti wetu kazi nyingi inafanyika maktabani. Tunasoma kwa kina vitabu na tahakiki mbalimbali kuhusiana na somo letu la utafiti pamoja na yale yanayohusu nadharia tunayotumia kueleza dhana mbalimbali. Tunashauriana na wataalam wa tafsiri hususan wahadhiri ili kupata uelewa zaidi kuhusiana na dhana ya ulinganifu. Tunasoma matini ya *Betrayal in the City* pamoja na tafsiri yake *Usaliti Mjini* ili kuchambua na kulinganisha data ya kimsingi. Imebidi tutumia mtandao kuhusiana na somo letu la utafiti.

# SURA YA PILI

## FAFANUZI ZA ULINGANIFU

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tunaliangalia kwa undani suala la ulinganifu kama linavyoeleweka katika utafiti huu. Ulinganifu katika matumizi yake ya kawaida ni mfanano au msabaha kati ya kitu na kitu kingine na katika tafsiri ulinganifu unachukuliwa kuwa mfanano ulioko kati ya kazi au matini chanzi na matini lengwa. Kwa kujikita katika uelewa huo, tunajaribu kutathmini uwezekano wa kuwepo kwa ulinganifu kati ya MC na ML.

### 2.1 Dhana ya ulinganifu

Dhana ya ulinganifu katika tafsiri imewahi kuelezwa kwa jinsi kadha wa kadha na wataalam tofauti katika nyakati tofauti. Tutaangalia baadhi ya fafanuzi na maelezo yao kwa nia ya kutaka kutumia maoni hayo kama kigezo cha kutathmini kuwepo au kutokuwepo kwa ulinganifu katika tafsiri ya kazi za kifasihi, Usaliti Mjini.

Ulinganifu umewahi kufafanuliwa kuwa ni fenomena jarabati inajitokeza wakati tunapolinganisha matini ya LC na ile ya LL. Katika uelewa huo wa fenomena jarabati, Catford anajaribu kubainisha kuwepo kwa aina kadhaa za ulinganifu kama vile ulinganifu wa kiumbo na ulinganifu wa kimatini. Ulinganifu wa kimatini unahusu ubainishaji wa msabaha ulioko kati ya sifa za kimatini za MC na

zile za ML, na hili ni jambo linatokana na chukulizi kwamba katika tafsiri sharti pawepo na msabaha wa aina fulani kati ya kazi chanzi na kazi lengwa. Lakini, hata hivyo, ni muhimu ieleweke kwamba kubainika kwa mfanano wa sifa yoyote ile ya kimatini ni sharti kutokane na ukweli kwamba sifa hiyo ndiyo iliyokusudiwa kubainishwa. Ulinganifu huu unaweza kutumiwa kama thibitisho kuonyesha jinsi matini zinavyofanana au kutofautiana. Kwa upande mwingine, ulinganifu wa kiumbo ni suala linaloelekeana na ulinganifu wa kiumbo, au kategoria za kiumbo kati ya LC na LL. Lakini zaidi, kinachoangaliwa ni mfanano wa kiuamili ulioko kati ya LC na LL katika viwango au kategoria mbalimbali, kwa mfano uamili wa miundo fulani ya ngeli fulani.

Ulinganifu wa kiumbo katika tafsiri ni suala linalofungamana na ulinganishaji wa jinsi maumbo ya lugha kati ya LC na LL yanavyofanya kazi. Kwa mfano, inawezekana kulinganisha na kutathimini jinsi ambavyo miundo ya sentensi, vishazi, virai, maumbo ya maneno au hata mofimu za LC na LL zinavyowiana katika uamili wao. Kwa hivyo, katika kuangalia ulinganifu wa kiumbo katika tafsiri, suala linaloibuka ni kule kukadiria kama lugha zinawiana katika misingi ya vipashio vidogo au vikubwa. Kwa vyovyote vile, ni sharti aina ya ulinganifu unaoshighulikiwa iwekwe wazi tangu mwanzo na sababu zake pia ziwekwe wazi. Kwa mfano, inawezekana kudai kwamba ulinganifu kati ya LC na LL unajitokeza kwa uwazi katika vipashio vikubwa kama vile sentensi kuliko ilivyo katika

vipashio vidogo kama vile mofimu au maumbo ya msamiati. Sababu kubwa inayoleta hali hii ni kwamba lugha zinatofautiana katika maumbo yao.

Tafsiri inahusu kuhamisha ujumbe unaolingana kutoka LC hadi LL kwa kuzingatia maana na mtindo unaotumika. Haya ni maoni ya Nida na Taber, (1969) ambao wanaelezea jukumu la mtafsiri kimsingi kama uhamishaji wa ujumbe kupitia urekebishaji mzuri wa msamiati na sarufi. Fauka ya hayo, mtafsiri anapaswa kung'ang'ania kufikia ulinganifu dhahiri badala ya kungangania kufikia hali ya kufanana. Kwa mfano, ulinganifu unaweza kufikiwa kupitia tafsiri ya kiisimu badala ya kutumia mwelekeo wa kitamaduni. Lengo kuu la kuchukua mwelekeo huu linatokana na maana kwamba lugha zote hutofautiana katika maumbo yao na kwa hivyo ili ulinganifu kudumishwa ni lazima umbo la LL kubadilishwa.

Tafsiri, kwa maoni ya Nida na Taber (1969), inahusu uhamishaji wa ujumbe na uhuishaji wa ujumbe unaolingana kimaana na kiuamili kati ya LC na LL kwa kuzingatia maana na mtindo unaotumika, lakini bila kupuuza miktadha ya upokezi wa matini lengwa. Maoni haya kwa njia kadha wa kadha yanaelekea kuwasilisha jukumu la mtafsiri na jinsi za uwajibikaji anazokabiliana nazo katika tafsiri. Kimsingi anawajibika katika uhamishaji wa ujumbe kupitia urekebishaji ufaao au mzuri wa msamiati na sarufi kwa nia ya kumwezesha mpokezi wa ujumbe kuupata ujumbe wenyewe. Mwelekeo huu unamtahadharisha mtafsiri kwamba anapaswa

kutambua kwamba kung'ang'ania ulinganifu ambao haujawekwa wazi ni shida kubwa. Kilichoko ni kwamba ni sharti mtafsiri aelewe aina za ulinganifu zinazowezekana na pia atambue kwamba hakuna kufanana katika tafsiri. Kwa sababu hii, mtafsiri anawajibika kutambua ni lini inakuwa muhimu kujenga ulinganifu wa kiisimu na kwa hivyo kuiruhusu tafsiri yake kuchukua mwelekeo wa kiisimu, au lini inahitaji ulinganifu wa kitamaduni na kwa hivyo kuchukua mfano, ulinganifu mzuri unaweza kufikiwa kupitia tafsiri ya kiisimu badala ya kutumia mwelekeo wa kitamaduni. Lengo kuu la kutambua mielekeo hii linatokana na ukweli kwamba lugha zote hutofautiana katika maumbo yao na katika mitazamo yao ya kilimwengu.

Ulinganifu, kwa maoni ya Beekman na Callow (1974), unabainika kutokana na ukweli kwamba watafsiri hulinganisha maneno mengi kati ya lugha hizo na katika viwango vya matumizi vinavyohusika. Wanafanya hivi hata kama wanajua kuwa lugha zinaweza kuwiana katika misingi ya maana na uamili japo kuna tofauti za kimsingi katika viwango vya miundo ya kifonolojia, kimofolojia, kisarufi na hata mipangilio ya msamiati. Hata kama huu ndio ukweli unaodhihirika, baadhi ya watafsiri na wasomi wamewahi kubuni chukulizi potovu ambapo wanachukulia, kwamba ulinganifu wa maana unaakisi ulinganifu wa miundo. Ithibati iliyoko inaonyesha kwamba chukulizi hizi si kweli. Japo kunaweza kuwepo na dhana zenye maana linganifu katika lugha mbili, matumizi na uamili wa dhana hizo hauwezi kulingana moja kwa moja. Tofauti hizi za kiuamili na kimatumizi

zinachochewa na kufungamana na uhalisi wa masuala ya kijiografia, kijamii, tajriba za kihistoria na hali halisi ya wakati uliopo. Hata kama zipo ithibati kuonyesha kwamba wakati mwingine lugha mbili zinaweza kutumia dhana moja kwa mtindo unaowiana katika lugha zote, au hata kama kuna uwezekano wa maneno kutoka lugha tofauti kuwa na mawazo na tajiriba zinazowiana, kuwiana huku hakuwezi kuwa ni katika kila hali na hatua. Ukweli uliopo katika tafsiri ni kwamba mtafsiri anawajibika kutumia lugha lengwa kwa kadri ya madai na kaida zake katika miktadha lengwa. Uelewa wa aina hii una maana kwamba ulinganifu katika tafsiri si kitu cha kijumla bali ni ulinganifu wa masuala dhahiri.

Kutafsiri kwa njia yoyote ile kunasababisha mabadiliko ya maumbo kadha wa kadha, hasa maumbo ya kazi chanzi inapolinganishwa na matokeo yake katika lugha lengwa. Larson (1984) anatambua ukweli huu kuwa ni jambo la msingi ambalo mtafsiri hukumbana nalo. Mabadiliko yanayotokea katika tafsiri mara nyingi huwa ya aina mbili; mabadiliko ya sharti na mabadiliko ya hiari. Larson anasisitiza kwamba madhumuni ya mabadiliko ya LC hadi LL yanatokana na haja ya kuleta uhamishaji wa maana kati ya lugha mbili husika huku mabadiliko hayo yakitilia maanani miundo ya kisemantiki inayohusika. Kitu kinachobainika hapa ni kwamba tafsiri inahusisha kwa njia kadha wa kadha uchunguzi na uchaguzi wa msamiati, miundo ya kisarufi, hali za kimawasiliano na miktadha ya kitamaduni ya LC. Hatima ya uchanganuzi na uchaguzi huu ni kuwezesha ujenzi upya wa maana kwa mujibu wa masharti ya kimsamiati, miundo ya kisarufi pamoja na

miktadha ya kitamaduni ya LL. Uelewa huu unabainisha kwamba kutafsiri kwokwote kule hakuna budi kuleta mabadiliko hata kama ni kidogo kiasi gani hivi kwamba hatimaye mabadiliko yoyote yale yanasababisha kutokuwepo kwa ulinganifu. Tunaposema kwamba pana ulinganifu wa kiumbo au kiuamili kati ya MC na ML ni kwa kukadria ukuribu na wala sio kulandana moja kwa moja kati ya matini zinazohusika au lugha zinazohusika. Vinginevyo ni kwamba hata kipashio kimoja kilichobadilishwa kinaweza kusababisha uwezekano wa kuleta maana tofauti isiyokusudiwa katika LC.

Kila mara, mtafsiri huwa anatafuta ulinganifu wa masamiati kati ya LC na LL ingawa jukumu hili huwa mchakato changamano unaofanya ulinganifu wa msamiati kuwa mgumu kuupata. Kwa upande mwingine, madhumuni ya kutafsiri kwa maoni ya Newmark (1988) ni kujaribu kuleta ulinganifu haswa katika tafsiri ya mawasiliano kama, vile matangazo, maagizo, propaganda, miongoni mwa mifano mingine. Kwa kujikita katika uelewa huu miitiko ya wasomaji kama vile *kununua bidhaa, kuhudhuria karamu n.k. huchukuliwa kama mafanikio makubwa* ya tafsiri. Kwa hivyo, mtafsiri huwa kila mara anajaribu kupata uwezekano wa ulinganifu katika LL, kama anavyoathiriwa yeye binafsi.

Suala la ulinganifu linatokana na mwingiliano changamano kati ya maana ya MC na thamani ya mawasiliano ya ML kwa maoni ya Neubert na Shreve (1992). Wasomi hawa wanakubaliana na maoni ya wasomi wengine kama vile Catford

(1965), Beekman na Callow (1974) na Larson (1989) kwamba maneno ya lugha ya kwanza na maneno ya lugha ya pili hayawezi kuwa na ulinganifu wa maana isipokuwa pale maneno yanahusiana katika viwango vya kitaaluma na kisayansi. Ukweli uliopo ni kwamba ulinganifu wa kimatini unawezekana lakini ni vigumu kupata ulinganifu wa kiisimu kwa kuwa maana ya neno ulinganifu haiwezi kuwa sawa na neno kufanana, kwa usemi mwingine, ulinganifu wa kimatini hutokea pale ambapo tunaweza kupata ulinganifu wa kijamii. Fauka ya hayo, majukumu ya kimawasiliano ya matini lengwa ni kuwasilisha taarifa kwa msomaji lengwa ambako matini chanzi haingeweza.

Kwa kujikita katika uelewa huu, matini hususan MC na ML hutoa taarifa sawa inayolingana kwa wasomaji wanaolingana katika hali ambayo inalingana na kuwezesha kuwepo kwa ulinganifu wa kimawasiliano. Kwa upande mwingine, ulinganifu unachukuliwa kama kipimo cha kukadiria ni kwa kiwango kipi matini huchukua nafasi ya matini nyingine kupitia tofauti za kiisimu na kitamanduni na kuleta uwezekano wa thamani ya kimawasiliano. Dhana ya ulinganifu inapoangaliwa kwa undani inabainika kama dhana ambayo imefunganisha mitazamo mbalimbali katika tafsiri kwa kuwa inahusiana na maswala ya kiisimu jamii, kiisimu, kisaikolojia, kihakiki na kimatini.

Matini chanzi inapowasilisha habari inazingatia athari ya mvuto, matarajio, maarifa na vikwazo vya hali ya hadhira ya utamaduni chanzi. Haya ndiyo maoni

yanayotolewa na Nord (1997) ambaye anaedelea kudai kwamba mtafsiri huchukua jukumu la kufahamisha hadhira nyingine ambayo iko katika hali na utamaduni mwingine tofauti habari iliyo katika MC. Dhima ya mtafsiri ni kupatia hadhira mpya ML inayoongozwa na chukulizi zake kama vile maarifa yake ya awali matarajio, mahitaji n.k. Ukweli uliopo ni kwamba mtafsiri anaongozwa na chukulizi tofauti sana na zile za mwandishi wa MC. Kutokana na ukweli huu, dhana ya ulinganifu ni dhana ambayo ni tuli na jukumu lake ni kueleza uhusiano unaolingana wa thamani ya mawasiliano kati ya matini mbili. Isitoshe, uhusiano huu unaweza kuangaliwa katika kiwango cha chini kama vile maneno, mafungu ya maneno, sentensi au miundo ya kisintaksia. Kwa hivyo, ulinganifu unahitaji ML ichukue jukumu sawa la kimawasiliano kama vile MC.

## 2.2.0 AINA ZA ULINGANIFU

### 2.2.1 Ulinganifu wa kiumbo

Ulinganifu wa kiumbo unahusika na kipengele cha LL kinachowakilisha neno au kifungu cha LC. Haya ni madai ya Nida na Taber (1969). Kwa maoni yao, mtafsiri ambaye ni mpokezi na chanzo kwa wakati mmoja hupokea ujumbe na kuutafsiri katika muktadha tofauti wa kitamaduni na kihistoria. Katika uelewa huo, mtafsiri huwa na matumaini makubwa kwamba ujumbe utamfikia mpokezi wa tafsiri kama alivyokusudia. Maneno yanayotumika kuelezea matukio katika lugha nyingi huwa ni maumbo ya vitenzi. Kwa upande mwingine, ikiwa neno au kifungu cha maneno kinachotafsiriwa katika LC ni nomino, lazima umbo la neno hilo au kifungu hicho

libadilishwe ili lichukue umbo la kitenzi cha LL na kwa kuchukua hatua hii maelezo ya matukio yanakamilika. Kwa vyovyote vile, kubadilishwa kwa maumbo kama haya ili kudumisha maana kunategemea masiala ya kiisimu na kitamaduni kati ya lugha mbili husika. Kwa mfano, mabadiliko ya kimaumbo kati ya Kiingereza na Kiswahili huwa makubwa kwa sababu ya tofauti za kimazingira na kitamaduni kati ya lugha hizi mbili.

Ulinganifu wa kiumbo unaweza kutokea katika viwango mbalimbali kama vile sentensi, kishazi, kirai, neno, mofimu n.k. (Catford, amenukuliwa tena ). Kwa kujikita katika uelewa huu, ulinganifu wa kiumbo katika lugha moja unaweza ukatokea pale ambapo kipengele na kategoria ya maneno katika lugha moja inalingana na lugha ya pili. Kwa mfano, tunaweza kupata ulinganifu kati ya Kiingereza na Kiswahili tunapotumia vivumishi pale tu kategoria hii itatumika kutoa habari zaidi juu ya nomino katika lugha zote mbili. Mathalan:

*MC: 4: Cold* *money*

*(Kivumishi)* *(Nomino)*

*ML: 5: Pesa* *baridi*

*(Nomino)* *(Kivumishi)*

Tunapochunguza mifano hii kwa undani tunapata thibitisho kwamba tofauti inayobainika ni mpangilio wa maneno tu. Jambo hili linatokana na sababu kwamba Kiingereza hufuata muundo wa kiima, kiarifu na yambwa tofauti na Kiswahili ambacho kinafuata mpangilio huru wa maneno kama vile:

*MC 34: Adika died for the truth*

*ML 46: Adika alikufa kwa anjili ya kupigania haki. Sentensi iliyotafsiriwa inaweza kuwa na mpangilio huru wa maneno kama vile kwa ajili ya kupigania haki, Adika alikufa.*

Kwa upande mwingine, lugha ya Kiingereza hutumia maumbo yanayotumika kama vibainishi kama vile '*an*', '*the*' na '*a*' ambavyo havitumiki katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo umbo kama vile '*The boy*' katika lugha ya Kiingereza linaashiria mvulana mahususi tofauti na Kiswahili ambako neno litakalotafsiriwa kama mvulana halitatupatia mwelekeo kama ule wa Kiingereza.

Kimsingi, tafsiri inahusu badiliko la umbo au kwa usemi mwingine tafsiri ni ubadilishaji kutoka hali au umbo moja hadi lingine kwa maoni ya Larson (amenukuliwa tena) umbo katika lugha linaweza kumaanisha maneno, mafungu, vishazi, sentensi, aya, n.k. yawe yamezungumzwa au yameandikwa, katika mchakato wa kutafsiri, umbo la LL huchukua nafasi ya umbo la LC kwa madhumuni ya kuhawilisha maana. Cha muhimu kukumbuka ni kwamba umbo ndilo linalobadilika lakini maana hubaki kama ilivyobainika katika LC. Kwa mfano, katika matini zetu za utafiti za *Betrayal in the City* na *Usaliti Mjini* tunaweza kuthibitisha haya.

*MC: 5: People say I Am mad*

*ML: 6: Watu wanasema kwamba mimi ni mwenda wazimu*

Umbo la sentensi hii limebadilika lakini maana imedumishwa katika sentensi hizi, yaani kuna mtu ambaye yuko katika hali ya wenda wazimu.

Tafsiri nzuri kwa maoni ya Larson ni ile inayofuata masiala matatu ambayo ni;

i. Kutumia maumbo ya kawaida ya LL kwa mfano '*bad road*' itakuwa barabara mbaya.

ii. kuwasilisha kwa wazungumzaji wa LL ujumbe ule ule vile ulivyoeleweka na wazungumzaji wa LC. Kwa mfano, ujumbe ulio katika sentensi ya Kiingereza 'The teacher is reading' ukitafsiriwa katika Kiswahili 'Mwalimu anasoma' ni kwamba kuna mtu ambaye ni mwalimu anayefanya kitu ambacho ni kusoma.

iii. Tafsiri nzuri pia inapaswa kuibua mwitiko sawa kama ulivyobainika katika MC. Kwa mfano, kama ni mwitiko wa kutovuta sigara katika eneo fulani, lazima mwitiko huu ubainike katika tafsiri.

Ili kufikia malengo haya, ni lazima kufanyika mabadiliko yanayofanyiwa LL ingawa maana haitegemei maumbo ya lugha moja na nyingine. Kwa hivyo, ni jukumu la mtafsiri kubuni matini ya LL (tafsiri) ambayo imebeba maana sawa na LC.

### 2.2.2 Ulinganifu wa uamili

Ulinganifu wa kiuamili hujumuisha ulinganishaji wa mfanano wa utendakazi wa lugha katika MC na ML. Kwa kawaida ni nadra sana kwa kipashio cha MC kuwa na maana iliyo sawa na kipashio cha LL katika fahiwa ya kiisimu ingawa vipashio

vyote viwili vinaweza kuwa na uamilifu ulio sawa katika hali moja. Haya ni maoni ya Catford (ibidi) wakati vipashio vyote vya LC vinapotafsiriwa hadi LL ni muhimu ikumbukwe kwamba kunatokea ulinganifu baina ya baadhi ya vipashio husika. Kwa mfano:

*MC: 73: Am I hearing right?*

*ML: 102: Ninasikia vizuri?*

Matini ya LL lazima iwe na uhusiano wa vipashio fulani vya matini ya LC. Kwa upande mwingine, ulinganifu wa kiuamilifu umeainishwa kwa namna nne na Nida na Taber (amenukuliwa tena) kama ifuatavyo;

i. Uamilifu wa mpangilio wa maneno unaofaa na unaowezesha maana kutambulika kwa urahisi
ii. Maumbo yawe yana uwezo wa kuleta mvuto wa kutambua ujumbe
iii. Uteuzi wa maneno yanayosaidia katika uelewa na ufahamu
iv. Matumizi ya maneno yanayoleta athari iliyo sawa na maumbo yenyewe ya maneno

Ili kufikia mambo haya, ni lazima kuwe na matumizi ya mitindo mbalimbali kama vile matumizi ya miundo rahisi ya diskosi, matumizi ya sentensi fupi, mpangilio unaofaa wa vishazi n.k.

Maana ya maneno, kwa maoni ya Beekman na Callow (1974), inaweza kuainishwa katika viwango vya umbo na uamilifu.

*MC: 10: May you die*

*ML: 13: Nawe pia upigwe fimbo ya mauti*

Kwa hivyo, ni muhimu mtafsiri yoyote abainishe maana ya maneno yote wakati wa mchakato mzima wa kutafsiri ili maneno hayo yafahamike kama yana maana ya kimaumbo au ya kiuamilifu. Wakati mwingine, mtafsiri anaweza kukumbana na neno katika LC ambalo halina neno lenye maana linganifu katika LL. Jambo kama hili linapotokea, ni dhima ya mtafsiri, kwa maoni ya Larson (amenukuliwa tena), kutambua maana ya neno hilo kama lilivyotumika katika kifungu au katika muktadha husika. Sababu ya kufanya hivi ni kwamba wakati mwingine mwandishi wa MC anaweza kulipa kipaumbele umbo la neno au uamili wake.

Kwa upande mwingine, umbo la neno mbwa linaweza kuelezwa kupitia masiala kama vile kipimo, umbo, rangi, n.k. Lakini uamilifu wake katika tamaduni fulani ni kutumika kama mlinzi. Wakati huo huo neno hili pia linaweza kutumika katika tamaduni nyingine kama mnyama mwindaji ilhali tamaduni zingine zitatumia umbo hili kwa minajiri ya mnyama kipenzi. Kwa hivyo, ni jukumu la mtafsiri kuelewa uamilifu wa umbo fulani katika LC ili maana inayobainika ihamishwe katika LL.

Neno katika lugha na utamaduni mmoja laweza kuwa na umbo na uamilifu sawa katika lugha na utamaduni mwingine. Kwa mfano,

*MC: 1: bowl*

*ML: 1: bakuli*

Maneno haya yana maumbo yaliyo sawa katika tamaduni za lugha zote mbili na uamili wake ni chombo cha kutumika nyumbani. Neno wakati huo huo linaweza kuwa na umbo sawa lakini matumizi yake ni tofauti kutoka tamaduni moja hadi nyingine na ni jukumu la mtafsiri kutambua uwezekano huu ili kukabiliana na maneno yanayojulikana kama 'marafiki wa uongo' katika mchakato wa kutafsiri. Haya ni maneno yanayoonekana kiumbo kama yanafanana kutoka lugha moja hadi nyingine lakini maana yake ni tofauti.

### 2.2.3 Ulinganifu wa kimuktadha

Muktadha unaweza kuelezwa kuwa ni ujumla wa mambo na uhalisi wote unaozunguka na kuathiri matumizi ya lugha kwa maoni ya Catford amenukuliwa tena). Kwa hivyo, ulinganifu wa kimuktadha unaweza kuelezwa kuwa ni msabaha, mfanano au ukaribu wa kimuktadha unaobainika wakati MC na ML zinapolinganishwa. Ulinganifu huo unaweza kuwa ni juu ya masuala ya kiwakati, kitamaduni, kiuamili,kihadhira, *n.k.* Hali kadhalika, uhalisi huu unaweza kujumuisha michakato ya kijamii, vitendo vya usemi, hali na mahusiano ya wasemaji pamoja na mitindo yao ya kibinafsi. Uhusiano wa kimuktadha unatokea wakati vipashio vya kisarufi au vya kileksika huhusika katika hali moja na vipashio vya elementi za kiisimu kati ya MC na ML. Kwa kujikita katika uelewa huu, vipashio vya kimuktadha vinabainika wakati kunatokea mabadiliko ya hali ya elementi zilizo na uhusiano wa maana ya kimuktadha. Hii ni kwa sababu lugha

mbalimbali huwa na tofauti za kimaumbo. Katika matini tunazoshughulikia, tofauti za kimuktadha zinaweza kuthibitishwa kama ifuatavyo;

*MC: 33: All the students want is his photograph printed in the local newspapers*

*ML: 45: Kile ambacho wanafunzi wanataka ni kuona picha ya Adika imechapishwa katika magazeti ya hapa nchini.*

Muktadha unaobainika katika MC haumtaji yeyote lakini mtafsiri amebadilisha muktadha kwa kutaja jina la mtu katika ML.

Kwa kujikita katika uelewa huu, tunaweza kudai kwamba katika baadhi ya nyakati na hali fulani fulani, ni vigumu kuupata ulinganifu wa kimuktadha kwa sababu mchakato wa kutafsiri unateua zile elementi zinazohusiana kihali kati ya LC na LL. Kwa maoni ya Larson (ibid), maana ya maneno huleta utata kwa sababu maneno huwa na maana zile za kimsingi na wakati huo huo kuna uwezekano wa maneno kuwa na maana za ziada. Maana ya kimsingi ni maana inayodhihirika wakati neno fulani linapotumika peke yake. Ikiwa neno lili hili linatumika katika muktadha na maneno mengine, maana ya kimsingi hubadilika. Kwa mfano maana ya maneno fulani katika matini tunazoshughulikia yataeleweka tu kwa sababu ya muktadha. Kwa mfano neno '*silent*' katika mfano huu linaekeweka kwa sababu ya kutumia muktadha.

*MC: 4: that is the voice of the brother of the silent one*

ML: 5: Hiyo ni sauti ya ndugu yake marehemu Adika.

Kwa hivyo, matumizi ya maneno yenye maana ya kimsingi huwa ni rahisi kuyatafsiri hadi LL na maana za maneno yenye ulinganifu sawa na maneno kama hayo lakini jambo hili linakuwa gumu wakati mtafsiri anapojikita katika mchakato wa kutafsiri maneno yaya haya wakati yanapotumika katika mikitadha tofauti. Hata hivyo, utambuzi wa mikitadha husaidia kupunguza utata wa maana katika matumizi ya lugha. Kwa mfano, matumizi ya kifungu kama 'Yeye ni mfupi' yana utata kwa sababu muktadha unaotumika haujabainishwa.

### 2.2.3. Ulinganifu wa kitamathali

Tamathali kwa maoni ya Mbatiah (2001) ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksi) ili kuleta maana mpya ya msisitizo.

Ulinganifu wa kitamathali ni ulinganishaji wa jinsi tamathali za lugha kati ya LC na LL zinavyofanya kazi. Kwa mfano, tunaweza kupata aina ya tamathali kama vile tashbihi katika LC. Tunapoilinganisha na ile ya LL, tunatafuta kama maana inayoibuka katika LC ndiyo haswa iliyohamishwa katika ML.

Tatizo kubwa la ulinganifu wa kitamathali ni utambuzi wa maana ya tamathali chanzi na jinsi ya kuiwasilisha katika LL. Haya yanatokana na matumizi ya tamathali mfu (tamathali ambazo zimeachwa kutumiwa) pamoja na matumizi ya nahau katika lugha. Matatizo ya kitamathali yanaweza kuepukwa kupitia matumizi ya maneno yasiyo na athari zozote za kitamathali kama vile

*MC: 23That, to them, was an eye for an eye, a tooth for a tooth; but then, they*

*were wrong.*

*ML: 31: waliponifanya hivyo, waliridhika kuwa eti walikuwa wamelipiza kisasi; lakini walikosea.*

Nahau ni mojawapo ya tamathali zinazopatikana katika lugha zote lakini zilizo na maana mahususi kimatumizi. Matumizi ya nahau kama vile *'he has a hard heart'* katika lugha ya Kiingereza yana maana ya mtu ambaye hajali mahitaji ya watu wengine. Nahau hii inapotumika katika lugha ya Kiswahili tunapata nahau kuwa na moyo mgumu ambako maana ile ile ya LC inaibuka. Hata hivyo, ni muhimu ikumbukwe kuwa matumizi ya tamathali katika tafsiri yanaweza kuwepo na wakati mwingine mtafsiri humbidi kutumia tamathali katika LL ingawa haikutumika katika LC Larson (amenukuliwa tena).

Matumizi ya maneno yanayohusiana kitamathali hujulikana kama mtindo wa metonimia. Mbinu hii inahusika na uhamishaji wa maana au sehemu ya maana na kuitumia katika mazingira mengine tofauti (Tuki 1990). Kwa mfano,

*MC: 39 You would be behind bars*

ML: 53 Ungekuwa umetiwa ndani.

Maana ya maneno '*behind bars)* imeamishwa na kuwa kufungwa jela)

Tafsiri ya moja kwa moja inapotumika katika tamathali kama hii maana iliyokusudiwa hupotoshwa katika ML na kwa hivyo ulinganifu wa kitamathali kudunishwa.

Mtafsiri anapaswa kuwa na ufahamu wa mawezekano ya ufumbuzi na ubunifu wa sitiari mpya katika utamaduni lengwa. Haya ni maoni ya Beekman na Callow (amenukuliwa tena.) Matumizi ya sitiari mpya huenda yakasababisha matumizi yasio ya kawaida ya lugha na kwa hivyo maana huathiriwa kwa sababu ya baadhi ya masiala kama vile tafsiri ya moja kwa moja na utata unaojitokeza.

### 2.2.4. Ulinganifu wa lugha kisarufi na kisintaksia

Tafsiri ya kisarufi ni tafsiri ambayo sarufi ya matini ya LL inachukua nafasi ya sarufi ya LC lakini kwa kudumisha baadhi ya maneno na kubadilisha mengine (Catford; amenukuliwa tena). Tunapojikita katika uelewa huu, ulinganifu wa lugha kisarufi unahusu jinsi vipengele mbalimbali vya LC vinavyoleta msabaha katika LL. Kama tulivyodokeza hapo awali, lugha ya Kiswahili huwa na mpangilio huru wa maneno tofauti na lugha kama vile ya Kiingereza.

Muundo wa kishazi katika lugha ya Kiingereza huwa SPCA ambapo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| S- | *Subject* | K – | *Kiima* |
| P- | *Predicator* | Kia- | *Kiarifu* |
| C- | *Complement* | Kj- | *Kijalizo* |
| A- | *Adjunct* | KE- | *Kielezi* |

Sentensi ya Kiingereza itafuata muundo wa SPCA wakati wote lakini sentensi itakayotafsiriwa hadi Kiswahili si lazima ifuate muundo wa kishazi cha Kiingereza

kwa sababu ya uhuru unaopatikana katika mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

*MC: 20: You can't afford to stick to your principles*

*ML: 27: Hustahili kushikilia vikali mashauri yako mwenyewe*

Sentensi ya Kiswahili inaweza kuandikwa kwa muundo tofauti kama vile, 'Mashauri yako mwenyewe hustahili kuyashikilia vikali'.

Viginevyo, tafsiri ya kisarufi inahitaji matini ya LL iwakilishe sarufi ya matini ya LC bora tu ipakishe vipashio vya leksika vya LC.

Ulinganifu wa kisarufi na kisintaksia unaweza kuwepo katika viwango mbalimbali hususan 'sentensi kwa sentensi, kirai kwa kirai, neno kwa neno n.k. (Catford: ibid). Hata hivyo, ulinganifu wa kisarufi na kisintaksia unaweza kuwekewa mipaka katika kiwango kimoja cha kisarufi kuanzia cha chini mpaka cha juu hususan neno hadi sentensi. Tafsiri ya neno kwa neno huwa imewekewa mipaka ingawa ulinganifu wa kimofimu unaweza kuweko wakati huo huo. Kirai katika LC chaweza kuwa na ulinganifu wa kishazi badala ya kirai katika matini ya LL. Mabadiliko ya viwango vya lugha (sentensi- sentensi, kirai- kirai, neno- neno au mofimu mofimu) sio tu mabadiliko yanayojitokeza wakati wa kutafsiri bali tunaweza kupata mabadiliko mengine kama vile ya miundo, ngeli, mifumo n.k. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza muundo wa sentensi huleta uwezekano wa kivumishi kuja kabla ya nomino tofauti na muundo wa Kiswahili mathalan.

*MC: 2: Stray Clansman*

*ML:2: Mwana ukoo aliyepotoka*

*MC: 36: Short call*

*ML: 45: Haja ndogo*

Wakati mwingine LC huenda ikawa na vibainishi kama vile vya Kiingereza ambavyo wakati wa kutafsiri hadi lugha kama ya Kiswahili ambayo haina vibainishi, basi tutapata tafsiri iliyo na ulinganifu kapa katika kiwango hiki.

*MC: 3: It is <u>the</u> noise he makes*

*ML: 4: Kelele anayofanya*

*MC: 23: That, to them, was <u>an</u> eye for <u>an eye</u>, <u>a</u> tooth for <u>a</u> tooth, but then, they were wrong.*

*ML: 31: Waliponifanya hivyo, waliridhika kuwa eti walikuwa wamelipiza kisasi, lakini walikosea.*

*MC: 38: The red guards*

ML: 51: Walinzi wekundu

**2:2:5 Ulinganifu wa kiisimu**

Ulinganifu wa kiisimu ni mfanano wa kiisimu kati ya lugha mbili tofauti unaojikita katika kuonyesha mikakati na taratibu zinazotumika kuwasilisha ishara za lugha moja kwa kutumia ishara linganifu za lugha nyingine ili kuhamisha maana iliyoko katika vitengo vya fonolojia, mofolojia, neno, sarufi na semantiki.

Ulinganifu wa kifonolojia kati ya LC and LL unaweza kutokea kwa njia tatu kama anavyobainisha Nida (1964) ambazo ni unukuzi wa vitengo vya maneno ya mkopo, kushughulika na maneno yanayofanana kifonolojia na mpangilio wa mtindo wa kimaumbo.

Tatizo la unukuzi hujikita katika tafsiri ya matumizi ya nomino halisi kutoka LC hadi LL lakini Nida (amenukuliwa tena) anapendekeza matumizi ya msamiati wa kukopa ili kutatua shida hii. Matatizo ya ulinganifu yanayohusika na fonolojia hutokea kwa sababu hakuna lugha mbili zenye mawezekano ya kuwa na sauti mbili zinazofanana kabisa. Nida anatoa pendekezo la kutatua tatizo hili kwa matumizi ya utohozi kama ifuatavyo kati ya MC ya *Betrayal in the City* na ML ya *Usaliti Mjini*.

| | |
|---|---|
| MC:68: | *Cadet* |
| ML: 95: | Kadeti |
| MC: 69: | *Captain* |
| ML: 95: | Kapiteni |
| MC: 69: | *Commander* |
| ML: 96: | Kamanda |
| MC: 71: | *Lieutenant* |
| ML : 99: | Luteni |

Miundo ya sauti za kifonolojia katika lugha fulani huenda inaleta uwiano sawa na ule wa Kiingereza ingawa majina katika tafsiri hayapaswi kutafsiriwa kama ilivyofanyika katika matini tunayoshughulikia kama vile:

| MC | ML |
|---|---|
| Jusper | Jaspa |
| Regina | Rejina |
| Nicodemo | Nikodemo |
| Boss | Bosi |

Katika kiwango cha mofolojia ulinganifu wa miundo ya maneno miongoni mwa lugha tofauti huhusisha sifa tatu ambazo ni uhusiano unaotokana na utata katika uundaji wa maneno, tofauti za ngeli na kategoria inayoletwa na maneno katika ngeli tofauti (Nida: amenukuliwa tena).

Utata katika uundaji wa maneno kama vile tafsiri ya Kiingereza hadi Kiswahili kama LL huhusisha matumizi ya mbinu tofauti kama vile kuelezea maana ya neno fulani. Kwa mfano, neno la Kiingereza kama vile 'judgement' linaweza kutafsiriwa kwa kutolewa maelezo kama vile 'Hukumu iliyotolewa'.

Wakati mwingine, mtafsiri anaweza kukumbana na kategoria za kimofolojia kama vile nambari (*tarakimu, takwimu*), dhamira, na hali n.k., ambako utata wakati wa kushughulikia ulinganifu kati ya lugha mbili hutokea, kama anavyodai Nida. Kwa

mfano, lugha nyingine kama vile zile za familia ya lugha zizungumzwazo sehemu za Ulaya na magharibi ya Asia hutumia nambari (tarakimu) kama sharti mojawapo ya matumizi ya lugha. Lugha zingine hazizingatii matumizi ya nambari kwa kujikita katika uelewa huu, nambari huwa kiwakilishi tu cha hali fulani tunapotumia mtazamo wa kisemantiki. Kwa mfano,. Matini tunazoshughulikia hufuata mtindo wa matumizi ya nambari kama vile;

*MC: 4:; Three cold silver coins*

*ML: 5: Sarafu tatu za fedha zenye baridi*

Kwa Upande mwingine, utata kati ya ulinganifu wa kimofolojia kama kipashio cha kiisimu huletwa na matumizi ya njeo. Kwa mfano,

*MC: 5: We'll need them*

*ML: 7: Tutawahitaji*

*MC: 10: may you die the way Adika did!*

*ML: 13: nawe pia upigwe fimbo ya mauti kama vile Adika alivyopigwa.*

Tofauti za kimofolojia kati ya Kiingereza na Kiswahili zinaleta hali ya kutokuwepo kwa ulinganifu wa aina hii katika matini husika.

Hali hushughulikia vile kitenzi kinavyofahamika kuwa ni timilifu yaani kimetimia au kinaendelea. Kwa mfano,

*MC: 20: Yes; he has recovered*

*ML: 27: Ndio, amepona*

Utata wa maana utatokea ikiwa mtafsiri atachukulia njeo kuwa hali.

Dhamira, kwa maoni ya Nida huonyesha utendakazi wa kitenzi kuonyesha ukweli wa matokeo, wajibu, kuhitajika kwa jambo, uwezekano wa jambo n.k. Jukumu haswa la dhamira katika lugha ni kuonyesha lengo la msemaji ambaye anaweza kuwa na nia mbalimbali kama vile kuarifu, kusihi na kuamuru. Kwa mfano:

***Swali***

*MC: 1: Who would have thought they would follow him even to his grave?*

*MC: 2: Ni nani angefikiri wangemfuata marehemu hadi mbele ya kaburi?*

***Amri***

*MC: 7: I told you to shut that mouth!*

ML: 9: *Nilikwambia ufunge huo mdomo wako!*

***Wajibu***

*MC: 71: You should know better than that*

*ML:99: Unatakiwa ufahamu zaidi kuliko hivyo*

Mtafsiri atakayetasfiri sentensi hizi katika lugha ya pili huenda akapoteza maana iliyokusudiwa ikiwa hatafahamu dhamira ya mwandishi wa MC kama tokeo la kisaikolojia.

Sauti huwa ni kipengele muhimu sana katika lugha ambako kama anavyosema Nida hidhihirisha uhusiano kati ya wahusika na tukio linaloashiriwa na kitenzi. Kwa mfano, mtenda 'alimpiga' na mtendwa 'alipigwa; Lugha zingine huwa

hazina vitenzi vya hali ya kutendwa na vinapotafsiriwa lazima marekebisho yafanywe ili maana iliyokusudiwa kufikiwa.

Kwa maoni ya Nida kuna lugha ambazo hutofautisha jinsia katika tungo za kisarufi kwa mfano Kifaransa, Kijereumani na Kiingereza, kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

*MC: 7: He thinks he has killed you*

*ML: 9: Anafikiri kuwa amekuua*

Sentensi iliyotafsiriwa haibainiki inamrejelea mwanamume au mwanamke.

Kwa hivyo, utata wa jinsia miongoni mwa lugha tofauti huenda ukapotosha maana inayopatikana katika MC.

Uhusika ambao hudhihirisha dhima ya maneno katika tungo huleta mawezekano ya kupotea kwa maana ya kazi au usemi chanzi kwa sababu dhana hii haipatikani katika lugha zote ulimwenguni.

Mawezekano mengine yanayoweza kuathiri maana hutokana na ukweli kwamba nafsi inayodhihirika katika LC haikutumiwa ifaavyo na mtafsiri. Kwa kujikita uelewa huu, ni muhimu mtafsiri atambue ya kwamba lugha nyingine hutofautiana katika matumizi ya nafsi za umoja na wingi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya lugha hutofautiana katika matumizi ya umiliki. *Matumizi ya dhana fulani kama vile baba, mama, binti, kwa maoni ya Nida (ibidi)* yanaleta maana kulingana na umiliki unaodhihirishwa na watumizi wa lugha fulani.

Mtafsiri huwa kila mara anajishughulisha na maana kama anavyodai. Newmark (1991). Kwa kujikita katika uelewa huu, ni muhimu maana itambulike kama kifaa muhimu ambacho kinabainisha vipengele mbalimbali vya *matini* ya LC vinavyolingana na matini mpya iliyotafsiriwa. Mifano iliyotolewa katika sehemu hii ya ulinganifu wa kiisimu inaonyesha tafsiri iliyotokana na watafsiri kama wasomaji.

**2.2.6 Ulinganifu wa kimaudhui**

Ulinganifu wa kimaudhui katika tafsiri ni swala linalofungamana na jinsi maudhui ya LC yanavyolingana na yale ya kazi lengwa. Tunapokuwa na maudhui ya ufisadi katika LC, tutajikita katika kulinganisha kama maudhui yaya haya yanabainika katika LL.

Mtafsiri anaweza kuwa na malengo tofauti tofauti ambayo ananuia kuyatimiza katika mchakato wa kutafsiri. Mojawapo ya malengo ya kutafsiri ni kupitisha ujumbe ule ule kama ulivyowasilishwa katika MC.

Kulingana na msomi Larson (1984), maudhui yaliyo katika MC yana uwezekano wa *kupitishwa hadi LL ikiwa mtafsiri atatumia mtindo unaofaa katika LL*. Kwa ujumla, maudhui ni mawazo makuu ambayo yanapatikana katika kazi ya kifasihi, iwe ni fasihi andishi au fasihi simulizi.

Ikiwa mtafsiri atatumia mbinu finyu ya kutafsiri, pana uwezekano wa kudhihirika kwa matatizo mbalimbali kama vile usonde katika lugha. Kwa mfano tafsiri finyu ya sentensi ya kiingereza ifuatayo italeta tatizo hili.

*MC: 4: Doga picks up the money from the bowl*

*ML: 5: Doga anachukua pesa kutoka kwa bakuli lililokuwa limewekwa juu ya kaburi.*

Mtafsiri yamfaa awe na uelewa wa matatizo ya tafsiri yanayohusiana na uwasilishaji wa ujumbe. Larson alinainisha baadhi ya matatizo haya kama ifuatavyo:

(i) Kuna ujumbe ulioko katika utamaduni wa MC ambao haujulikani na wazungumzaji wa LL.

(ii) LL hutumia mbinu tofauti za kuhusisha ujumbe ulioandikwa mbeleni na jinsi ya kuunganisha ujumbe mpya katika matini husika.

(iii) Kila lugha ina mchakato wa matarajio ambapo maneno au vifungu fulani vinatarajiwa kufuata maneno gani.

(iv) Kuna uwezekano wa kulingana kwa mpangilio wa uziada na uaminifu miongoni (*kati ya lugha mbili*) mwa lugha mbili tofauti.

(v) Maana ambayo haijaelezwa wazi katika LC itaelezwa wazi katika LL au kinyume cha haya.

Maana inayopatikana katika matini fulani inategemea utamaduni wa lugha husika. Kwa usemi mwingine wasomaji wa LL watafasiri maana kulingana na kanuni pamoja na kaida za utamaduni wao. Hii inatokana na ukweli kwamba hawawezi kukaribia tajiriba za mwandishi wa MC na kwa hivyo ni jukumu la mtafsiri kuelewa ujumbe ulioko katika MC kulingana na tajiriba zake.

Kwa upande mwingine, mtafsiri anaweza kueleza katika utangulizi wa tafsiri yake dhana au istilahi zisizofahimika katika LL ili maudhui anayokusudia kuyawasilisha katika ML yadumishwe kama yanavyobainika katika MC.
Kwa maoni ya Larson, mtafsiri anaweza kutumia mbinu ya maelezo ili kufanikisha lengo lake la kuwasilisha maudhui kama anavyodai Larson (ibidi) iwapo matumizi ya dhana zilizo katika LC hayafahamiki katika utamaduni wa LL.

Ni muhimu kwa hivyo mtafsiri asome na kupata uelewa wa ndani ili maudhui yanayobainika katika MC yaweze kubainika katika LL. Kwa mfano:
*MC: 29: Brutes! Murderers! Beat up my innocent sister until she lost hearing in one year. Why beat a woman? Why didn't they beat me?*

*ML: 38: Mahayawani! Wauaji! Walimpiga dada yangu asiyekuwa na hatia mpaka sikio lake moja likapoteza uwezo wa kusikia. Kwa nini walimpiga mwanamke? Kwa nini hawakunipiga mimi?*

Maudhui yanayobainika katika matini hizi mbili yanalingana kwa sababu yote yanaashiria dhuluma inayotendewa wanawake Ingawa dhuluma hii imekuwa ikiendelezwa kwa muda wa miaka mingi, ni muhimu kwa mtafsiri kutambua mabadiliko ya kihistoria ambayo yanaleta mabadiliko ya kimaudhui kama vile kutokea kwa dhuluma dhidi ya wanaume.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

## 2.2. 7 HITIMISHO

Katika sura hii tumefafanua dhana ya ulinganifu kwa ujumla Kwa upande mwingine, tumetoa ithibati kwamba katika matini mbili husika ambazo ni MC na ML huwa kuna uwezekano wa kuwepo au kutokuwepo kwa aina mbalimbali za ulinganifu dhahiri kama tulivyojadili. Kwa kujikita katika uelewa huu, yale yote tuliyofaidika nayo yatatupatia mwelekeo utakaotuwezesha kutathimini aina mbalimbali za ulinganifu kati ya MC ya Betrayal in the city na ML ya *Usaliti Mjini*. Hili ndilo lengo letu katika sura inayofuata.

# SURA YA TATU

## 3.0 TATHMINI YA AINA ZA ULINGANIFU

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tunathimini aina mbalimbali za ulinganifu kama zinavyobainika kwa maana ya kuwepo au kutokuwepo kwao kati ya MC ya *Betrayal in the City* na ML ya *Usaliti Mjini.*

Tunachanganua kwa undani sababu ambazo zinachangia kupatikana au kutopatikana kwa ulinganifu kati ya MC na ML kwa kujikita katika nadharia ya mwitiko wa msomaji Aidha, tutajadili vipashio mbalimbali vinavyopatikana katika lugha kwa ujumla na kazi za kifasihi hasa.

Kwa upande mwingine, tutanukulu mifano mbalimbali kutoka katika matini tunazorejelea ili kuweza kujadili uwezekano wa kuwepo au kutokuwepo kwa ulinganifu.

### 3.2 Ulinganifu wa kiumbo

Mtafsiri yeyote hutekeleza jukumu lake la kutafsiri kazi yoyote ile baada ya kupitia mchakato wa kusoma matini fulani. Maana inayobainika baada ya hatua hii inategemea masiala mbalimbali kama vile uwezo wake kama msomaji pamoja na tajiriba zake. Kutokana na hali hii maana inayobainika kutoka kwa mtafsiri mmoja kama msomaji ni tofauti kabisa na maana inayoibuka wakati mtafsiri mwingine

anaposoma kazi ile ile. Kwa hivyo, maana inayoibuka kutokana na usomaji wa kazi moja na watu tofauti haiwezi kuwa moja kila wakati.

Kwa mfano, ulinganifu wa maumbo ya lugha kati ya LC na LL kwa kawaida hauwi wa moja kwa moja, hasa pale lugha zinazohusika zinapokuwa hazitoki katika jamii za lugha moja. Kiswahili kina jinsi zake za kuambisha maneno na kwa njia hiyo kujenga maana mpya. Watafsiri wa *Usaliti Mjini* wamelipuuza jambo hili kiasi kwamba wanalazimika kuingiza ama mifumo ya Kiingereza katika ML au kulazimisha maelezo marefu yanayotatiza mtiririko wa maongezi.

mfano;

*MC: 1: Wooden bowl*

*ML: 1: Bakuli lililotengenezwa kwa mabao*

Hali hizi za kulazimisha maumbo au maelezo katika ML zinaishia kujenga uhalisi mpya kama vile usemezano unaojikokota. uibukaji wa maana tofauti kutokana na ubadilikaji wa maumbo ya lugha. Jambo hili lina athari nyingi katika ufasiri wa ML ikikumbukwa kwamba Kiswahili ni lugha inayopanua maana za maneno kutokana na taratibu za uambishaji. Mbali na hayo, kule kung'ang'ania kujenga ulinganifu kwa kufungika katika taratibu za lugha chanzi, kunafilisha uwezekano wa kuwepo kwa ulinganifu wa kiuamili.

Umbo a lugha ya Kiingereza *wooden* limetafsiriwa kama mabao kwa sababu ya watafsiri wakijaribu kuleta ulinganifu wa viambishi katika neno bao. Neno

*wooden* lina viambishi tamati 'en' lakini neno mabao lina viambishi vitangulizi 'ma' na kuleta matumizi yasiyo ya kawaida ya umbo hili katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ulinganifu unaopatikana hapa wa kiumbo haupaswi kuwepo kwa sababu ya tofauti za kaida za lugha kati ya Kiingereza na Kiswahili.

Watafsiri wa Usaliti mjini wametafsiri maumbo mengine na kuibua maana tofauti kabisa na ile iliyokusudiwa na mwandishi wa MC mawezekano kama haya yanatokana na chukulizi zao kuhusu maana ya maumbo fulani. Matokeo yake ni kusababisha uundaji wa maumbo tofauti kimaana na *ile* ya LC. Mfano ufuatao unathibitisha haya:

*MC: 1: Lives among us even now*

*ML: 2:anaishi kadamnasi mwetu hata sasa*

Watafsiri walitumia tajiriba yao kutafsiri umbo *among* kama kadamnasi ambalo halilingani kamwe. Kwa maoni yetu, watafsiri walijaribu kuleta thamani ya ujumi katika lugha ya Kiswahili bila kujali athari ya kupotea kwa maana inayopatikana katika LC. Matini ya LC imetumia neno *among* kumaanisha 'miongoni' lakini ulinganifu uliotumiwa uko nje ya maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC.

Mfano mwingine ufuatao unaonyesha pia ukosefu wa ulinganifu kati ya MC na ML

*MC: 49: Jusper, tell your cousin that life is not a straight line*

*ML: 67: Jaspa, mweleze binamu yako kuwa tuko hapa duniani kwa muda tu*

Maana iliyofasiriwa na watafsiri kutokana na MC imetupatia tafsiri ambayo haikulenga maana chanzi kamwe katika mafungu haya. Watafsiri walipatia neno la mtu 'Jusper' utohozi hili liwe 'Jaspa' kwa kujaribu kuleta ulinganifu ingawa majina ya watu hayawezi kutafsiriwa. hii kwa maoni yetu inatokana na sababu za kutaka kuleta muundo wa silabi unaopendelewa katika lugha ya Kiswahili yaani konsonati vokali (KV).

Vitenzi katika lugha huchukua nafasi kubwa sana kwa sababu ni vigumu kupata sentensi sahihi katika lugha yoyote ambayo haina kitenzi. Kitenzi 'tell' katika MC kimetafsiriwa kama 'mweleze'. Neno 'mweleze' linatokana na neno la Kiingereza 'explain'. Kwa upande mwingine, kitenzi cha Kiingereza 'tell' kinapotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kitakuwa mwambie. Maana inayoibuka kutokana na vitenzi hivi hususan mwambie na mweleze haiwezi kuwa sawa.

Kwa upande mwingine umbo la MC *'life is not a straight line'* limekosa ulinganifu kabisa kwa sababu watafsiri wamehamisha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Jambo ili limetokana na ufasiri wa maana na watafsiri kama wasomaji kwa vile maana inayopatikana katika ML huwa tofauti kabisa kutegemea wasomaji mbalimbali. Kutokana na hali hii, ni vigumu sana kupata maana zinazofanana kutokana na wasomaji mbalimbali kwa vile maana inayoibuka baada ya mchakato wa kusoma hutegemea ufasiri wa wasomaji.

Aina hizi tofauti za ufasiri wa maana huwa na athari kubwa katika tafsiri. Hii ni kwa sababu tafsiri yoyote itategemea uwezo wa watafsiri katika kuibua maana kila mara wanapojikita katika mchakato wa kusoma.

### 3.3 Ulinganifu wa uamili

Ulinganifu wa kiuamili kama tulivyokwisha jadili katika sura iliyopita ni mfanano wa jinsi lugha inavyotenda kazi kati ya MC na ML.

Uamilifu wa lugha pia hutegemea tajiriba na uwezo wa mtafsiri kwa sababu ingawa kuna kamusi zinazosaidia katika uelewa wa maana, wakati mwingine maana huwa vigumu kubainika. Kwa mfano:

*MC: 18: dead right, shake my five, shake my five*

*ML:24: hiyo ni kweli kabisa. nipe mkono ule tano zako. Kula tano zako tafadhali*

Uamili wa lugha katika kifungu cha MC unaonyesha dhamira ya kusalimiana. Tajiriba imewafanya watafsiri wa *Betrayal in the City* hadi *Usaliti Mjini* kuangazia uamilifu huu katika MC. Kutokana na kifungu kilichoko hapa juu, maana iliyoibuka katika tafsiri huenda ikaashiria kitu kingine tofauti sana na lengo la mwandishi wa MC. Kwa maoni yetu watafsiri wanapohamisha maana ya '*shake my five,* kuwa 'kula tano zako' wanafanya haya kutokana na ufasiri waliopata wakati wa mchakato wa kutafsiri.

Kifungu kifuatacho kinaonyesha pia ulinganifu wa kiuamili kuhusiana na ngeli kati ya lugha mbili tofauti hususan Kiingereza na Kiswahili.

*MC: 33: I don't, I will never have rest.*

*ML: 44: Sihitaji kupumzika. Sijawahi kupumzika*

Lugha ya MC imetumia maneno matatu yaliyo na uamili wa nafsi ya kwanza umoja (1) Kitenzi (*do)* na neno *"not"* lililo na uamilifu wa kuwa hasi. Uamilifu huu wote unabainika kupitia neno la Kiswahili '*Sihitaji*'.

Hii ni kwa sababu kitenzi cha kiswahili huwa na uamilifu mbalimbali kama vile njeo, nafsi, dhamira na hali.Mfano ufuatao pia unaonyesha ulinganifu wa kiuamili kati ya MC na MC.

*MC: 10: May you die the way Adika did!*

*ML: 13: Nawe pia upigwe fimbo ya mauti kama vile Adika alivyopigwa.*

Ulinganifu wa kiuamili unaopatikana katika LL unaonyesha matokeo ya kifo kinacholetwa na hali mbili tofauti. Kifo kinachotokea katika MC hakifahamiki kilitokana na nini katika muktadha huu. Kwa upande wa maana ya ML, inaonekana kwa maoni yetu kuwa kifo cha Adika kinasababishwa na nguvu fulani tunapojikita katika muktadha huu.

Kama tulivyojadili katika sura yetu ya awali, ni muhimu kwa mtafsiri kutumia mtindo unaowezesha maana ya maneno kubainika. Haya yanaweza kufikiwa kupitia matumizi ya mtindo na muundo rahisi unaosaidia kuhamisha maana ya LC hadi LL.

## 3.4 Ulinganifu wa kimuktadha

Muktadha kama tulivyojadili katika sura iliyotangulia ni ujumla wa hali na uhalisi wote unaoizunguka kazi ya kifasihi, mambo ambayo kwa njia kadha wa kadha yanachangia sio tu kueleweka kwa kazi husika bali pia kufasirika kwa kazi hiyo. Kwa hivyo, ulinganifu wa kimuktadha ni msabaha ulioko kati ya kazi chanzi na kazi lengwa. Kwa njia hii tunaweza kusema kwamba matendo na maigizo yanayojitokeza katika kazi chanzi yanajengeka katika miktadha dhahiri, miktadha hii ndiyo inayoshawishi uteuzi wa lugha na jinsi inavyopangwa na kwa njia hiyo maana zinazozuka kutokana na mipangilio hiyo. Suala hili la miktadha limepuuzwa kwa kiasi kikubwa na watafsiri wa *Usaliti Mjini*. Katika mifano ifuatayo, tutaonyesha jinsi miktadha ilivyopuuzwa na kwa jinsi hiyo kuzua ukosefu wa ulinganifu.

Tofauti ya miundo ya lugha mbalimbli huleta hali ngumu ya kuwepo kwa ulinganifu kati ya lugha mbili zilizo na tofauti za kitamaduni, kikaida na hata kihistoria. Watafsiri wa *Usaliti Mjini* wamejaribu kuleta ulinganifu wa kimuktadha

kulingana na uwezo na tajiriba zao ingawa ni jambo gumu kupata kama inavyobainika kupitia mifano ifuatayo;

*MC: 4 Doga picks up the money from the bowl*

*ML: 5 Doga anachukua pesa kutoka kwa bakuli lililokuwa juu ya kaburi*

*MC: 7 His eyes were full of sleep*

*ML: 10 Macho yake yalikuwa na usingizi mwingi hivyo basi kusharabu Wekundu*

*MC: 40 Does any of you care for coffee?*

*ML: 54 Kuna mmoja kati yenu 'atakayejali nikiwatengenezea kahawa?*

Katika mfano wa kwanza, muktadha katika MC unahususishwa na pesa zilizokuwa ndani ya bakuli. Uwezo wa watafsiri wa *Usaliti Mjini* waliibua maana lengwa kufuatia ufafanuzi wa muktadha chanzi ili maana ya ML iweze kufahamika kwa uwazi. Jambo hili linaleta ukosefu wa ulinganifu wa kimuktadha kwa kuwa, hapo mwanzoni mwandishi wa MC alikuwa ametoa maelezo ya mahali bakuli lilipokuwa na kwa hivyo hakukuwa na maana ya kurudia jambo hili.

Mfano wa pili unatuonyesha maana inayojitokeza kulingana na tajiriba za watafsiri. Wao walikuwa na ufahamu kwa sababu ya tajiriba zao kuwa macho yote ambayo yanaonyesha hali ya kuwa na usingizi lazima yawe na wekundu. Tajiriba ya watafsiri inaleta ufafanuzi wa muktadha wa MC kutokana na ufasiri

waliyopata. Wanapofikia hatua ya kuhamisha maana watafsiri wanapanua muktadha kwa 'matumaini' kwamba maana ya MC itaeleweka vyema katika ML.

Ukosefu mwingine wa ulinganifu wa kimuktadha unabainika katika mfano wa tatu. Maana inayojitokeza katika MC ni ya kwamba mhusika alitaka kujua kama kuna yeyote aliyejali kunywa kahawa. Hatuwezi kujua kutokana na MC kama kahawa ilikiwa tayari au la lakini kutokana na tajiriba ya watafsiri wao walichukulia kahawa haikuwa imepikwa na kwa hivyo wakaleta matini ambayo haina ulinganifu wa kimuktadha.

Kifungu cha maneno '*Does any of you care for coffee?*' kinaweza kuchanganuliwa kama kina maana tofauti. Mojawapo ya maana hizi ni kuwa, huenda kahawa ilikuwa imepikwa na kilichohitajika ni kunywa tu peke yake. Pili, maana iliyofasiriwa na watafsiri inaweza kubainika kwa sababu huenda kahawa haikuwa imepikwa.

Ulinganifu wa kimuktadha huwa vigumu kupatikana kutokana na tofauti za kiutamaduni kati ya LC na LL. Wakati mwingine inawabidi watafsiri watumie muktadha tofauti na ule wa LC ili maana inayopatikana katika MC iweze kufafanuliwa upya na hivyo kufanya kueleweka kwa maana ya ML kuwa rahisi. Miktadha lengwa isipochukuliwa mkakati kama huu huenda matokeo ya tafsiri yaani ML ikawa ni vipande tu vya vipashio vya lugha visivyojenga maana yoyote.

## 3.5 ULINGANIFU WA KITAMATHALI

Ulinganifu wa kitamathali ni mfanano wa kimakusudi wa ukiushi wa matumizi lugha kati ya LC na LL. Lugha zinazotofautiana kwa sababu ya kihistoria, kiutamaduni kimazingira na kimuundo huwa zinatumia tamathali ambazo ulinganifu wake ni vigumu kuupata. Kwa mfano lugha inayotumia tamathali zinazohusiana na hali za kimazingira kama vile barafu huenda itatumia tamathali zinazohusishwa nayo. Kwa upande mwingine, tamathali kama hizi huwa ni vigumu sana kueleweka au kutafsiriwa katika lugha ambayo haitumii hali ya mazingira ya barafu. Masiala kama haya ndiyo yanayoleta ugumu wa kupatikana kwa ulinganifu kati ya MC na ML tunazoshughulikia katika utafiti huu. Kwa mfano:

i. *MC:3 A mouse does not share a bowl with a cat*

   *ML:4 Panya hawezi kutumia sahani moja na paka*

ii. *MC: 15 Get out of my sight now!*

   *ML: 20 Toka machoni mwangu sasa*

Mifano hii miwili inaonyesha ulinganifu wa moja kwa moja wa kitamathali unaotokana na hali ya kutaka kujaribu kuleta mfanano kati ya MC na ML wakati wa mchakato wa kutafsiri. Jambo hili linaweza kuleta uwezekano wa kupunguza athari za kitamathali zilizonuiwa na mwandisi wa MC na kwa hivyo ML nayo ikakosa athari ya kitamathali.

Hata hivyo watafsiri wa *Usaliti Mjini* walijaribu kutafsiri baadhi ya tamathali kwa kufuata miundo ya LL bila kuifanya ionekane ikifuata kaida za LC. Kwa mfano,

*MC: 36 Thank you, it's a short call*

*ML:45 Asante, ni haja ndogo*

Kifunga cha MC 'short call' kinalingana na kifungua cha kitamathali haja ndogo katika LL. Kutokana na haya, inadhihirika kuwa pana uwezekano wa kutokea au kutotokea kwa ulinganifu wa kitamathali kati ya lugha mbili tofauti. Hii huenda ikasababishwa na uwezo wa watafsiri kuzimudu lugha mbili tofauti.

Aidha michakato ya kiutamaduni kati ya lugha moja na nyingine huleta tofauti za kitamathali. Mazingira pia huchangia pakubwa katika uundaji wa tamathali. Kwa hivyo, ni nadra sana kupata ulinganifu wa kitamathali kati ya LC na LL ambako mazingira yake ni tofauti kabisa. Kwa mfano:

MC: 47: Since we sit on the fence

ML: 64: Hatuonyeshi kuwa na msimamo wowote.

LC inapotumia mazingira ya ua katika muktadha huu inawakilisha maana ya ndani ya kitamathali. Iwepo watafsiri wangelichukulia suala kama hili kijuujuu maana iliyokusudiwa na tamathali chanzi haingepata mfanano wake katika ML.

Kutokana na hali kama hizi za kitamathali, inafaa watafsiri kuchunguza kwa undani maana halisi ya tamathali za LC wanapojikita katika mchakato wa kusoma ili maana itakayohamishwa ilete athari kama ile iliyokusudiwa na mwandishi wa MC.

### 3.6 Ulinganifu wa lugha, kisarufi na kisintaksia

Huu ni ulinganifu unaohusu jinsi vipengele mbalimbali vya LC vinavyoleta hali ya kuwa na ukaribu katika LL.

Kama tulivyosema katika sura iliyopita muundo wa lugha ya kiswahili na Kiingereza ni tofauti mno. Lugha ya Kiswahili huwa na mpangilio huru wa maneno ambako sentensi fulani yaweza kuanzia na kirai chochote kinachotumika katika sentensi husika. Mfumo kama huu huwa ni nadra kutumiwa katika baadhi ya lugha Kiingereza kikiwemo. Jambo hili linaleta ugumu wa kuwa na ulinganifu wa kisarufi kati ya MC na ML.

Watafsiri wa Usaliti Mjini wametumia mikakati mbalimbali ili kujaribu kuleta ulinganifu wa kisarufi katika kazi lengwa. Mojawapo ya mikakati hii ni kugawanya sentensi mbalimbali ili ufasiri wa maana uweze kubainika. Hali hii inatokana na sababu kwamba, watafsiri ni wasomaji na ni lazima wajitafutie mtindo wao wa kuifasiri maana ya kazi chanzi ili waihamishe katika ML. Kwa mfano:

*MC: 1: A wooden bowl sits at the centre of the grave, in it, a few silver coins*

*ML: 1: Katikati ya kaburi hili kuna bakuli lililotengenezwa kwa mabao.*

*Ndani ya bakuli hili kuna sarafu chache za fedha.*

*MC: 6: We got to restore human dignity, right?*

*ML: 7: Tunapaswa kurejesha heshima ya kibinadamu. Sawa?*

Sentensi hizi zinatuonyesha mifano mwafaka ya mikakati inayochukuliwa na watafsiri wanapokumbana na hili ya kutaka kuleta ufasiri wa maana kutoka ML hadi MC.

Sentensi za MC zinapopanuliwa, lengo la watafsiri huwa ni kujaribu kutatua matatizo ya kutokuwepo kwa ulinganifu. Haya yanapofanyika, matokeo yake ni kuleta ulinganifu unaosaidia kueleweka kwa maana ya MC. Watafsiri wakati mwingine wanapokwepa kuchukua mkakati kama huu huwa vigumu sana kutafsiri lugha moja hadi nyingine. Kwa upande mwingine, maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC huwa ni vigumu kuihamisha na matokeo yake ni kuwepo kwa matini mbili tofauti kabisa kimaana.

Aidha, watafsiri wanatumia uwezo wao kujaribu kuleta ulinganifu wa kisarufi na kisintaksia wakati wa kutafsiri lakini matokeo yake yanakuwa ni tafsiri ya moja kwa moja katika MC na ML. Kwa maoni yetu, mkakati kama huu unaweza kutumia na watafsiri kama wasomaji kwa kusudi la kutaka kuleta tafsiri za aina mbalimbali katika ML. Kwa mfano:

*MC: 6: She is far away in the City. Where is your father?*

*ML: 8: Yuko mbali sana mjini. Wapi baba yako?*

Watafsiri wa Usaliti Mjini kama wasomaji wametumia mkakati wa kuunganisha sentensi mbili katika MC na kuifanya kuwa moja. Haya yanafanyika kwa sababu

ya kuhamisha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Vipengele fulani vya sentensi za MC huenda zikakosa maana zinapotafsiriwa katika ML.

kwa usemi mwingine, vipengele kama hivi vinapotafsiriwa vitaonekana kama vinaninginia tu katika ML bila ya kusaidia lolote katika ujenzi wa maana lengwa. Ni muhimu kwa hivyo kwa watafsiri kama wasomaji kuunganisha sentensi kama hizi ili pawe na ulinganifu wa maana ya kisarufi katika ML. Kwa mfano:

*ML: 38 Am, in the wrong place? I hope not!*

*ML: 51 Inaonekana nimepotea au nini*

Fauka ya hayo watafsiri wametumia mkakati wa kufutilia mbali vipashio fulani katika sentensi ili kujaribu kuleta ulinganifu wa kisarufi. Kwa mfano:

*MC: 20 You can't afford to stick to your principles, No not here*

*ML: 27 Hustahili kushikilia vikali mashauri yako mwenyewe*

Kipashio cha kisafuri 'No. Not here!' kimefutiliwa mbali. Hii ni kwa sababu uamilifu wake katika sentensi ya ML umechukuliwa na viambishi vya sentensi inayotangulia. Kwa hivyo, kipashio hicho kikitumika tena kitaleta hali ya uchovu na marudio katika ML.

Watafsiri pia wamefutilia mbali baadhi ya kategoria za maneno katika ML. Mkakati kama huu umechuliwa pia kwa lengo lilo hilo katika mfano ufuatao:

*MC: 8 Trust and Obey*

*ML: 10 Amini Utii.*

Ingawa lengo la watafsiri wa MC kama wasomaji ni kujaribu kuleta ulinganifu, matokeo yake wakati mwingine yanaweza kuleta ML ambayo inaleta maana tofauti na ile ya MC. Kwa mfano:

Kufutiliwa mbali kwa kiunganishi 'and' kumeleta tofauti ya maana ya kisarufi katika sentensi hizi kwa sababu sentensi ya MC inaonyesha masharti mawili husussan 'Trust' na 'Obey' ilhali sentensi ya ML inaonyesha uhusiano kwa sababu mtu anapaswa aamini ili atii na kwa hivyo hakuna ulinganifu wa kisarufi.

Tofauti za miundo ya lugha kati ya Kiingereza na Kiswahili zinaleta tofauti ya mipangilio ya kategoria za kisarufi. Uamilifu wa kivumishi ni kutoa sifa zaidi juu ya nomino katika lugha. Kivumishi katika lugha ya Kiswahili huja kabla ya nomino tofauti na mfumo wa Kiingereza kama ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| *MC: 10:* | *Big* | *Coward* |
| | *(Kivumishi)* | *(Nomino)* |
| *ML: 13:* | *Mwoga* | *Mkubwa* |
| | *(Nomino)* | *(Kivumishi)* |

Kutokana na mifano tuliyojadili hapa juu, ni dhahiri kwamba watafsiri wa *Usaliti Mjini* kama wasomaji wametumia mikakati mbalimbali ya kuleta ulinganifu wa kisarufi. Kwa mfano wametumia mikakati ya kufuta na kupanua vipashio fulani. Lengo la kutumia mikakati kama hii katika tafsiri ni haja ya kutaka kuleta ulinganifu wa kisarufi kati ya lugha mbili tofauti. Zaidi ya hayo, uhamishaji wa

maana kutoka MC hadi ML lazima utekelezwe kwa mbinu kama hizi kwa kujaribu kuweko kwa Ulinganifu. Hii ni baadhi ya mikakati iliyotumiwa na watafsiri wa *Usaliti Mjini* kama wasomaji wa MC ya *Betrayal in the City*.

**3.7 Ulinganifu wa kiisimu**

Tunajadili vipashio mbalimbali vya kiisimu kati ya MC na ML vinavyobainisha ulinganifu wa kiisimu. Isimu ni taaluma inayochukua mwelekeo wa kisayansi katika uchunguzi wa lugha. Lugha ya Kiingereza hubainisha tofauti ya kijinsia tofauti na Kiswahili ambacho hakitofautishi jinsia. Maana hubainika kijinsia kwa sababu ya muktadha katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

*MC: 23: He was Jesus and I Pilate*

*ML: 31:Yeye alikuwa Yesu nami Pilato*

Matumizi ya kitenzi 'alikuwa' kutokana na kitenzi cha MC '*He was*' yanatupatia maana iliyo tofauti. Sababu ya haya ni kwamba, lugha ya kiingereza hutumia viwakilishi vinavyobainisha jinsia tofauti na Kiswahili.

Lugha ya Kiingereza ni tofauti sana na lugha ya Kiswahili kimofolojia. Kwa maoni yetu, viambishi vitangulizi au vifuatilizi katika maneno ya lugha ya Kiingereza huwa na maana fulani. Watafsiri wanaosoma matini fulani hutumia mikakati ya aina tofauti ili waweze kuleta ulinganifu kati ya lugha mbili husika.

Kwa mfano, watafsiri wanaweza kutumia mkakati wa maelezo ili kufanikisha ulinganifu wa viambishi katika maumbo ambayo havipatikani katika lugha ya Kiswahili mathalan:

*MC: 18 .....Meteorological department*

*ML: 24.....Idara ya hali ya hewa na anga*

Uwezo na tajiriba za watafsiri wa tamthilia ya *Usaliti Mjini* unaonyesha kwamba, wao walifutilia mbali baadhi ya sauti ili walete ulinganifu katika ML. Mfano ufuatao unathibitisha haya:

*MC: 29 You senseless brute!*

*ML: 39 We! Hayawani mshenzi!*

Watafsiri wamegawanya sentensi ya MC na kuifanya kuwa sentensi mbili. Kwa upande mwingine umbo la neno 'You' katika LC linapotafsiriwa linapaswa kuchukua nafsi ya pili yaani 'wewe' lakini watafsiri wa matini husika wamefutilia mbali sauti fulani na kaucha sauti 'we' badala ya 'wewe'. Neno hili 'we' halijulikani kama linachukua nafsi ya pili au limetumika kama kihisishi.

Vipengele fulani vilivyotafsiriwa vinaonyesha tafsiri dhaifu ambako vipashio vya kimofolojia hafikutafsiriwa kwa njia mwafaka.

Kwa mfano:

*MC: 32 A small room with main and kitchen doors.*

*ML: 43 Katika chumba kidogo kuna mlango mmoja mkuu na mwingine mdogo wa jikoni.*

Maana iliyoibuka wakati wa kutafsiri sentensi ya MC kutokana na uwezo wa watafsiri kama wasomaji inabainika kuwa tofauti sana na ile ya ML. Tajiriba ya watafsiri inaonyesha ya kwamba walibadilisha umbo la neno 'doors' kutoka hali ya wingi hadi umoja. Mbinu kama hii huathiri maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC na kwa hivyo kuna uwezekano wa kutokuwepo na ulinganifu wa maana.

Alama za uakifishi huchukua nafasi kubwa pia katika utekelezaji wa maana katika lugha. Hata hivyo, watafsiri kama wasomaji wamebadilisha baadhi ya alama za uakifishi. Mbinu kama hii huenda ikaleta mawezekano ya kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya MC na ML. Hii ni kwa sababu tunapata uelewa kwamba, kila alama ya uakifishaji huwa na maana tofauti katika mchakato wote wa matumizi ya lugha.

Alama ya kistari kifupi imetumika katika MC lakini inabadilishwa na alama ya kusisitiza kutokana na maana iliyoibuka wakati wa kutafsiri kulingana na uwezo wa kuimudu lugha kwa watafsiri kama wasomaji. Kwa mfano:

*MC; 32:* *You and your brother are the only people I have in the world, But Mosese is in. That leaves you –you alone –to build or destroy me.*

*ML; 44:* *Wewe na ndugu yako ndio watu wa pekee nilio nao kunifariji humu duniani, lakini Mosese yuko gerezani sasa wewe ndio umebaki! Wewe peke yako! Kunijenga au kunibomoa.*

Uamilifu wa kipengele 'wewe peke yako' hauonekani kuleta maana sawa kama ile iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Hii ni kwa sababu alama ya uakifishi ya kistari kifupi inatumika ili kufafanua maana zaidi. Tofauti na haya, watafsiri wametumia alama inayorejelea maana ya kutoa amri katika matumizi ya lugha.

Mifano tuliyoijadili hapa juu inabainisha mikakati inayochukuliwa na watafsiri katika mchakato wa kutafsiri MC. Vipashio mbalimbali vya MC vinapotafsiriwa vinaweza kupanuliwa, kufutwa au kupunguzwa vinapohamishwa katika LL. Lengo la kujikita katika stadi hizi za kimikakati ni kwa kujaribu kuleta ulinganishaji wa kiisimu baina ya MC na ML.

### 3:8 Ulinganifu wa Kimaudhui

Maudhui kwa maoni ya Mbatia (2001) huitwa pia yaliyomo. Haya hawa ni mawazo, fikira, dhamira na hisia zinazowasilishwa na kazi ya kifasihi. Kwa hivyo, ulinganifu wa kimaudhui ni suala linalofungamana na jinsi mambo yaliyomo katika LC yanauleta msabaha katika LL.

Tamthilia iliyotafsiriwa imejitokeza na maudhui mbalimbali kama yanavyobainika pia katika MC. Kwa mfano:

Maudhui ya Utamaduni - Imani za kitamaduni kati ya MC na ML zinabainika kupitia matumizi ya lugha kama vile;

*MC: 3:* *But if they should know what has happened, they will whisper and*

*say we ignored tradition. They will boycott my son's shaving ceremony. Please Doga, let us report this matter.*

ML; 4: *Lakini ikiwa watafahamu yaliyotendeka, watanongonezeana na kusema tulipuuza mila zetu. Watu watasusia sherehe ya unyoaji wa nywele ya mtoto wangu. Tafadhali Doga, tuipeleke habari hii kwa wakuu wa utawala ili wapate kujua kinachoendelea hapa.*

Tajiriba ya watafsiri kama wasomaji imeibua maana ya ulinganifu wa maudhui kuhusiana na mila na desturi za jamii husika hususan unyoaji wa nywele unaotendeka baada ya mazishi. Adika anapozikwa kulingana na mila na desturi ya jamii husika kunahitajika kutekelezwa mila hii kama mojawapo wa michakato yake ya kijamii. Matini zote mbili zinawasilisha maudhui haya.

Maudhui mengine yanayojitokeza katika MC na ML ni ya dini kwa sababu ya kuzingatia maana ya kifungu cha maneno kifuatacho:

*MC: 12: I have nothing else to offer you; (handing him a pocket Bible) take this, May god open your eyes to the suffering of your people.*

*ML: 16: Sina kitu kingine chochote cha kukupatia; (Akimpatia Biblia ndogo ya mfukoni) Chukua zawadi hii! Na mwenyezi mungu afunue macho yako uone matatizo ya watu wako.*

Ingawa watafsiri kulingana na uwezo wao kama wasomaji wameongezea maneno mengine, maana ya kimaudhui ya kidini imebainika kupitia matumizi ya neno

bibilia linaloashiria dini ya Kikristo. Kwa upande mwingine, tunaona vile wanyonge wanavyobaki na Mungu tu wa kumlilia wakati wa dhiki wakati viongozi wanapoendelea kutumia asasi mbalimbali za kudhulumu watu kama vile askari.

Uozo katika jamii unabainika pia katika MC na ML. Uozo huu unajitokeza mwanzoni mwa kitabu tunapolitazama kaburi la Adika aliyeuwawa akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu cha Kafira.

Uozo huu unaendelea kutekelezwa hata baada ya mhusika Jusper kukamatwa ambako anaachiliwa baada ya kufahamika kwamba wazazi wake wameuawa kama inavyodhihirika hapa:

*MC: 20: Yes; he has recovered, but he has nothing to go back to. His parents were found dead in their hut.*

*ML: 27: Ndio, amepona lakini hana chochote cha kujivunia anaporudi nyumbani. Wazazi wake walipatikana wamekufa ndani ya kibanda chao.*

Kwa upande mwingine, usaliti kama maudhui umejitokeza katika MC na ML kwa mfano:

**MC: 73:** *Mulili: No reason. You can kill*

*Jere: Do you agree that he should be got rid off?*

*Mulili: Kabisa! One, he take everything in his hand. Two, he spoil the economic of Kafira. Three, he rule too long. Change is like a rest. Four, he kill Kabito.*

***ML: 102:*** *Mulili: Hakuna sababu. Unaweza kuua*

*Jere: Unakubali ya kwamba anaweza kumalizwa?*

*Mulili: Kabisa! Kwanza, anaweka kila kitu mkononi mwake. Pili, anaharibu kiuchumi ya Kafira. Tatu, anatawala muda mrefu sana. Mabadiliko ni kama mapumziko. Nne, anamwua Kabito.*

Mulili alikuwa akishirikiana na kiongozi wa Kafira kujipatia utajiri kupitia njia za ufisadi na hata mauaji lakini mhusika huyu anamsaliti Boss ili ajitoe mashakani kama vile mhusika Petero alipomkana Yesu katika bibilia takatifu.

Inavyobainika katika mifano hii ni kwamba ulinganifu wa kimaudhui unawezekana bora tu uwezo wa watafsiri kama wasomaji watafsiri MC kwa miundo ya lugha inayosaidia kujenga maana ile ile iliyokusudiwa na mwandishi wa MC.

Ulinganishaji wa maudhui baina ya MC na ML unaonekana kama aina mojawapo za ulinganifu zinazowezekana kati ya matini mbili husika. Haya pia yanawezekana kwa sababu ya watafsiri kujikita katika utekelezaji wa mikakati inayotumika kuleta ulinganifu. Kwa mfano, watafsiri wametumia mkakati kama vile wa maelezo wakati dhana ya MC haitumiki katika LL.

# SURA YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

Katika tasnifu hii tumechunguza kwa undani maswala yanayohusiana na dhana ya ulinganifu katika tafsiri. Katika sura ya kwanza tumetoa mwongozo wa tasnifu hii, upeo wa tasnifu, tatizo la utafiti na nadharia tete: Vilevile tumerejelea yaliyoandikwa kuhusiana na tatizo letu la utafiti na tukaelezea misingi ya kinadharia pamoja na njia za utafiti tulizozitumia katika kazi hii.

Katika sura ya pili tumetoa fafanuzi za dhana ya ulinganifu kwa ujumla na kisha tukajadili aina mbalimbali za ulinganifu huku tukitoa mifano kutoka katika matini zetu za utafiti.

Katika sura ya tatu tumejikita katika swala la kutathimini aina mbalimbali za ulinganifu huku tukitoa mifano mbalimbali kutoka kazi chanzi na kazi lengwa ili kubainisha uwezekano wa kuwepo au kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya MC na ML.

Fauka ya hayo, tumefanya uchanganuzi wa matatizo ambayo hudhihirika katika matini iliyotafsiriwa. Tumejikita katika tamthilia iliyotafsiriwa ya *Usaliti Mjini* (1994) ambayo ni kazi mojawapo miongoni mwa zingine zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Utafiti huu umechunguza aina mbalimbali za

ulinganifu katika tafsiri hususan ulinganifu wa kiumbo, kiuamili, kisarufi, kimuktadha, kiisimu, kitamathali na kimaudhui.

Tumepata ya kwamba dhana ya ulinganifu ni dhana ambayo maana yake haijafafanuliwa kwa uwazi kabisa na wanadharia wengi. Wengi wa wanadharia wamejadili maana ya ulinganifu kwa kujikita katika misingi fulani kama vile kueleza ulinganifu kwa kujikita katika leksia, muktadha, uamili na mengineyo.

Katika uafiti wetu pia tumepata ya kwamba, watafiti walitumia mikakati mbalimbali inayotumika katika tafsiri. Baadhi ya mikakati hii ni kama vile kupanua baadhi ya vipashio fulani katika matini ili maana iliyo katika MC iweze kuhamishwa vyema. Aidha, watafsiri wametumia mkakati wa kufuta baadhi ya vipashio Fulani kwa lengo la kuleta ulinganifu katika ML. fauka ya hayo, watafsiri wametumia mbinu ya kuunganisha sentensi fulani kwa matarajio ya kukamilisha maana iliyo katika sentensi moja bila kuleta utata wa kimaana. Hii ni mifano ya mikakati iliyotumika katika matini ya *Usaliti Mjini* kama tafsiri ya MC ya *Betrayal in the City*.

Kwa upande mwingine, dhana ya ulinganifu imechanganuliwa kwa misingi dhahiri. Katika kazi ya kifasihi ya *Usaliti Mjini* na imebainika kuwa, isipokuwa katika ulinganifu wa kimaudhui, ni vigumu sana kuwepo kwa aina zingine za ulinganifu kati ya Kiswahili na Kiingereza tunaporejelea kazi yetu ya utafiti.

Tunapendekeza ya kwamba wasomi wa taaluma ya tafsiri wajikite katika uchunguzi zaidi kuhusiana na dhana hii kwa vile mwelekeo kama huo utasaidia katika kutathimini kazi zinazotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Fauka ya hayo, ni muhimu kutafiti na kuchunguza sababu zinazochangia hali hii ya kutokuwepo kwa aina nyingi za ulinganifu katika kazi zilizotafsiriwa ili watafsiri waweze kupata mwanga wa kuwawezesha kutekeleza jukumu la kutafsiri kwa kuzingatia mbinu mwafaka zitakazosaidia katika uimarishwaji wa mchakato wa kutafsiri.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Aidha, tunasadiki ya kwamba mwongozo tulioutoa katika sura ya kwanza hasa katika kipengele cha nadharia tuliyoitumia kutawachochea wachunguzi na watafiti wengine wa taaluma ya tafsiri kufanya uchanganuzi wa maswala yanayodhihirika katika matini watakazoshughulikia. Tunapendekeza tafiti zitakazofanyika kuhusiana na dhana ya ulinganifu katika miaka ijayo zifanywe kwa kuegemea matumizi ya nadharia za kisasa.

Madhumuni tuliyoyaweka mwanzoni mwa kazi hii yetu ya utafiti yametimizwa. Tumejadili dhana ya ulingaifu ili kubainisha kwamba kutafsiri ni jambo linalotegemea uelewa wa kina wa dhana ya ulinganifu. Tumebainisha ya kwamba matatizo na kasoro za tafsiri zinazojitokeza katika tafsiri ya *Usaliti Mjini* zinahusishwa na uelewa potovu wa dhana ya ulinganifu.

Nadharia tete zetu zimeweza kupimwa kulingana na utafiti tulioufanya. Imedhihirika kwamba watafsiri hawajafanikiwa kuleta aina fulani za ulinganifu katika kazi iliyotafsiriwa. Hii ni kwa sababu, mkabala wa fenomenolojia katika nadharia tuliyotumia ya mwitiko wa msomaji inabainika kwamba watafsiri kama wasomaji hawakufaulu sana kuleta aina mbalimbali za ulinganifu katika tafsiri ya kazi ya kifasihi ya *Usaliti Mjini*. Hii kwa maoni yetu imetokea kwa sababu ya mwelekeo uliochukuliwa na watafsiri kama wasomaji kwa kujaribu kuhamisha kaida za LC katika LL.

Tunapendekeza ya kwamba uelewa wa dhana ya ulinganifu unapaswa kupewa kipaumbele ili vipengele vyote vinavyohamishwa kutoka LC hadi LL vitekelezwe kwa njia mwafaka..

Hata hivyo, tunatoa maoni ya kwamba kuwepo au kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya MC na ML hakuwezi mnyima msomaji hamu yake ya kuisoma kazi ya kifasihi iliyotafsiriwa.

# MAREJELEO


Ali, C.W. (1981) "*The Problem of Translating from English into Swahili or Exemplified by V.O.K News Items,*" (Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Armstrong, N (2005) *Translation, Linguistics, culture,* AFrench-English Handbook, Multilingual Matters, Clevedon.

Baker, M (1992) *In Other Words, a Course Book of Translation*, Routledge, London.

Beekman, J. na Callow J. (1974) *Translating the Word of God,* Zondervan, Grand Rapids.

Bressler, C. (ed) (2003) *Literacy Criticism an Introduction to Theory and Practice, Prentice*

Catford, J.C. (1965) *A Linguistic Theory of Translating*, Oxford University Press, London.

Cook, G. (2003) *Applied Linguistic,* Oxford University Press, china.

Crystal D. na Davy, D. (1967) *Investigating English Style*, Dai Nippon Printing Co. International Hong-kong.

Fawcett, P. (1997) *Translation and Language: Linguistic Theories Explained*, St. Jerome, Manchester.

Gentzler, E (2001) *Contemporary Translation theories*, Multilingual Matters, Clevedon.

Guenthener, F. na Guenthner, M (1978) Meaning and Translation, Duckworth, London

Gutknectht, C. na Rolle, J.L, (1996) *Translating by Factors*, State University of New York: Albany, New York.

Hermans T. (ed) (1985) *The Manipulating of Literature: Studies in Literally Translation.* Groom Helm Ltd. Burrel Row Bekenham Kent.

Hofman, T.H.R. (1993) *Realms of Meaning*, Longman New York

Kelly L.G. (1979) *The True Interpreter*, Basil Blackwell, London

Kirk, R. (1986) *Translation Determined*, Clarendon Press, Oxford.

Larson, M, (1975) *A manual for Problem Solving in Bible Translation*. Summer Institute of Linguistics, Dallas, Texas.

__________., (1984) *Meaning – based Translation: A guide to Cross- Language Equivalence* University Press of America, New York.

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi*, Standard Textbooks Graphics and publishing, Nairobi.

Mulila, A.K. (2005) *Muala na Mshikamano Katika Kiswahili, Umuhimu wake katika Uchanganuzi wa Riwaya ya Vipuli vya Figo*, (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutie, E.K. (1997) *Sanaa Katika Tafsiri, matatizo na Athari Zake* (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi

Mwansoko, H.J.M. (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu,* Tuki, Dar es salaam.

Neubert, A. na Shreve, G.M. (1992) *Translation as Text*, Kent State University Press, Kent.

Newmark, P. (1981) *Approches to Translation*, Pergamon Press.

Newmark, P. (1988) *A Textbook of Translation*, Prentice Hall, New York.

__________., (1991) *About Translation*, Multilingual Matters Clevedon.

Nida, E.A. (1964) *Towards A Science of Translating, with SpecialReference to Principles and Procedures Involved in Bible, Translating,* Leiden Brill, Netherlands.

Nida E.A. na Taber, C. (1969), *The Theory and Practice of Translation*, United Bible Societies, Leiden.

_________ (2001) *Contexts in Translating*, Benjamins Publishing, Amsterdam.

Onguko, S.A. (1999) . *A Comparative study of cohension in academic and newspaper Texts* (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cah Kenyatta).

Shitemi, N.L. (1990) *Mawasiliano katika Tafsiri, Uteuzi wa Mtafasiri,* (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi).

Tuki (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya lugha*, Dar es Salaam.

____ (2006) *English-Swahili Dictionary*, Book printing Services Ltd, Mauritius.

_____ (1990) *Kamusi ya Isimu na lugha*, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Wamitila, K. (2006) Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele vyake, Focus, Nairobi.

Wolfreys, J (ed), (2001) *Introducing Literary Theories*, Edinburgh University Press, Edinburgh.

Zaja, J.O (1986) *Fasihi Tafsiri, Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili, (Matatizo na Athari Zake* (Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

_________ (2006) Siting Text, *Culture, Context and Pedagogy In Literary Translation: A Theorization of Translation in Cultural Transfer with examples from selected texts in Kiswahili* (Mswada wa PHD Chuo Kikuu cha Kenyatta).